**Putin** atoa neno uasi wa Wagner

UKURASA 4



MAUAJI DADA WA BILIONEA MSUYA

**Polisi** wadaiwa kuchukua dola za mshtakiwa

UKURASA 4



Ukurasa 14

Kulinda hifadhi kwa mtutu kunavyoweza kumalizwa

Ukurasa 13

Kelele mafuta kupikia, TARI inapozijibu kwa kuleta alizeti mpya

Nipashe TESA

Jumanne Juni 27, 2023

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 12

Uhaba, ukosefu vitabu ulivyokoma shuleni kupitia maktaba mtandao

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

NAO NI UNYANYASAJI

Usichukulie poa kutumia majina ya vitu, wanyama kukejeli watoto huwaathiri

Adhabu kwa watoto zilizopitiliza ni ukatili na unyanyasaji. PICHA: MTANDAO

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Juni 27, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581354

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




# Mwanasheria Mkuu Serikali aibuka sakata la Bandari

UKURASA 2



## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**VIJANA WATAKA UKOMO WA UBUNGE**

VIJANA wamesema kutokuwapo kipengele kinachoweka ukomo wa nafasi ya ubunge kunachangia vijana wengi wasipate nafasi...


## Bajeti mikopo elimu ya juu, vyuo vya kati sasa Bil.800/-

UKURASA 2



SIMBA KUTOROKA HIFADHINI

## Waziri Utalii awapa tahadhari watu wanaotembea usiku

UKURASA 4

**MICHEZO** SIMBA, BEKI MCAMEROON KIMEELEWEKA UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa kwenye mazungumzo na Ujumbe wa Shirika la Kimataifa la Christian Blind Mission (CBM) ukiongozwa na Mkurugenzi Mkaazi nchini Tanzania, Nesia Mahenge (kulia kwa Rais), Mkurugenzi wa Maendeleo Jumuishi wa CBM, Dominique Schulkopthen na Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Albert Kombo, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mwanasheria Mkuu wa Serikali aibuka mjadala wa DP World

**Mwandishi Wetu,** DODOMA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali (AG), Jaji Dk. Eliezer Feleshi, amejitosa katika mjadala wa uwekezaji wa Kampuni ya Dubai ya DP World unaotarajiwa kufanywa Bandari ya Dar es Salaam, akisema kuna upotoshaji mkubwa usio na tija kuhusu suala hilo.

Akizungumza kwa mara ya kwanza katika mazungumzo maalum na mwandishi wetu jijini Dodoma jana, Jaji Feleshi alisema kuwa upotoshaji huo unaweza kuifanya Tanzania ionekane inabagua wawekezaji kutoka nchi fulani.

"Mtu anasema mkataba ni wa miaka 100 na hiyo ilikuja hata kabla Bunge halijaazimia. Wengine wanasema ni mkataba wa maisha. Unatafuta hicho kipengele cha maisha unapekua kifungu kimoja mpaka mwisho, hakuna," alisema Feleshi.

Alisema ikumbukwe kuwa Tanzania tangu miaka ya nyuma, miongo mitatu, miwili iliyopita ilisaini makubaliano kuhusu matumizi ya mabaraza mengine ya kimataifa ya utatuzi wa migogoro na haijajiondoa.

Kadhalika, alisema kuna mambo ya msingi ili mtu awekeze hasa kwenye mtaji mkubwa ni lazima aangalie mfumo wa sheria ya nchi kama inavyosema ibara ya 24(2) inazuia utaifishaji wa mali ya mtu isipokuwa kwa matakwa ya sheria na mtu ili awekeze ni. lazima nchi iwe na amani ya kutosha.

Alionya pia kuwa lugha za kibaguzi zinazotolewa na baadhi ya watu dhidi ya wawekezaji kutoka nchi fulani zinaweza kuharibu sifa ya Tanzania kama taifa linaloongoza kuvutia watalii kutoka ukanda wa Afrika.

"Je, sasa tunataka tujenge mazingira ya kuwatia hofu wawekezaji kwamba nchi yetu haitaki wawekezaji?" Alihoji Jaji Feleshi.

Kadhalika, alisema Tanzania imekuwa inajulikana ni nchi isiyofungamana na upande wowote miaka mingi na inayokaribisha wawekezaji kutoka sehemu zote duniani.

"Leo unapoanza kuona Waarabu ni kama shida, unachagua (wawekezaji watoke) wapi?" alihoji.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali pia alikanusha hoja kwamba Bandari ya Dar es Salaam inauzwa akisisitiza hakuna kipengele chochote katika mkataba kati ya Tanzania na Dubai (Inter Governmental Agreement - IGA) kinachozungumzia uuzwaji wa bandari.

"Tunaposema bandari imeuzwa, je, ni kweli imeuzwa? Kile kiambatisho kimeeleza maeneo ya uhusiano kwa mujibu wa ile ibara ya 4, ni kwenye gati ngapi kati ya ngapi na hizo zinazobaki ni ngapi," alisisitiza.

Alifafanua kuwa Bunge limepitisha azimio la ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai katika eneo la bandari, lakini hakuna mkataba wowote ambao umetiwa saini kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na Kampuni ya DP World.

"Mpaka sasa TPA haijaingia makubaliano au mkataba wowote na DP World kwani muda wake haujafika," alisema.

Pia alikanusha alichokiita upotoshaji unaoenezwa na baadhi ya watu kuwa Tanzania au TPA haitoweza kujitoa katika makubaliano itakayoingia na DP World.

"Kama kuna kushindwana framework (msingi) imeshawekwa. Tangu mwanzo katika preamble (utangulizi wa makubaliano) imetajwa mikataba itakayokuja kuingiwa kama HGA (Host Government Agreement -HGA) na project agreement (mtakaba wa uendeshaji wa magati ya bandari)," alisema.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliongeza kuwa katika mkataba ambao TPA itatia saini na DP World, mwekezaji huyo atapewa masharti mahsusi na malengo ya utendaji na endapo mwekezaji ataonyesha ufanisi, anaweza kuongezwa maeneo mengine kwa mujibu wa matakwa ya serikali.

Jaji Feleshi amewahi kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DDP) na Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

# Mikopo elimu ya juu, kati yaongezeka hadi bil. 800/-

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema serikali imeongeza mikopo ya elimu ya juu, lengo sasa ni kufikia Sh. bilioni 800 kwa mwaka ujao wa fedha.

Huku akitaja kipindi hicho kinatarajiwa kuwa na wahitaji wapya kutoka vyuo vya kati, vya afya na ufundi, Dk. Mwigulu amesema ni kasi ya ongezeko la bajeti hiyo, sasa kwa wastani wa Sh. bilioni 200, ndani ya miaka miwili ya fedha.

Kwa mujibu wa bajeti hizo za miaka miwili iliyopita, katika mwaka wa fedha 2021/22, kulitengwa Sh. bilioni 500 na kwa mwaka uliofuata 2022/23, zilitengwa Sh. bilioni 570, lakini kutokana na upungufu wa kibajeti, Bunge lilifanya mapitio, bajeti ikafikia Sh. bilioni 654.

Akijibu hoja mbalimbali za wabunge baada ya mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2023/24 bungeni jana, waziri huyo alisema lengo ni kuwezesha watoto wa kitanzania kunufaika na elimu ya kati.

Dk. Mwigulu pia alisema serikali iliwasilisha mapendekezo ya kuongeza tozo ili kupata fedha za kusomesha watoto maskini walio na sifa ya kusoma vyuo vya kati lakini uwezo ni mdogo.

Alisema kuwa tangu Aprili mwaka huu matokeo ya kidato cha tano yalipotangazwa serikali imelazimika kujenga madarasa, ili kuhimili ongezeko la watoto waliofaulu kutoka 75,000 hadi 192,000.

Alisema serikali imeweka utaratibu wa kupeleka wanafunzi vyuo vya kati kwa kuwa shule za sekondari hazitoshelezi kuchukua wanafunzi wote waliofaulu, hivyo mpango wa serikali wa kuondoa ada katika vyuo hivyo unalenga kumwondolea mzigo mzazi, ili mtoto huyo apate ujuzi utakaolisaidia taifa.

KUKUBALI TOZO

Dk. Mwigulu pia aliwataka Watanzania kukubaliana na ongezeko la tozo iliyowekwa na serikali ikiwamo la Sh. 100 katika kila lita ya mafuta ya dizeli na petroli na Sh. 20 katika kila kilo moja ya saruji kwa kuwa fedha hiyo inakwenda kusomesha watoto wao.

Alisema Watanzania watakuwa wameonyesha mfano mbaya kwa kizazi hicho kama watashindwa kuwalipia watoto hao ada kwa sababu tu wanataka kujilimbikizia mali ilhali walipata elimu ya juu kwa kupitia mikopo hiyo.

"Watoto wa Watanzania ni watoto wetu ni lazima tubebe mzigo, ninawaomba Watanzania wote tukubaliane na maoni hayo hata kama yanatuongezea mzigo, yanatuongezea mzigo kwa ajili ya watoto wetu. Hizo ni fedha ambazo zinakwenda kutengeneza taifa lililo bora kwa sasa na miaka inayokuja," alifafanua Dk. Mwigulu.

Aliwasihi wananchi wasiirudishe nchi miaka ya nyuma ambayo licha ya mwanafunzi kufaulu vizuri na kuchaguliwa kuendelea na elimu, shule zilikuwa hazitoshi.

Katika mjadala huo, wabunge wengi waliishauri serikali kuongeza kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, ili wanafunzi wote wanaofaulu hasa kidato cha tano wapate shule.

Vilevile, waliishauri serikali kuhakikisha vyuo vya kati vyote vinaondolewa ada ili kuongeza wataalamu nchini na kuzalisha wataalamu wa kutosha kulitumikia taifa katika kada mbalimbali.



Mafundi wakiendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa Uwanja wa Mashujaa, katika mji wa Kiserikali Dodoma, unaotarajiwa kukamilika Juni 30, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana wataka ukomo wa ubunge

**Na Elizabeth Zaya**

VIJANA wamesema kutokuwapo kipengele kinachoweka ukomo wa nafasi ya ubunge kunachangia vijana wengi wasipate nafasi hiyo na kuendelea kushikiliwa na watu wale wale kwa kipindi kirefu.

Vijana hao walitoa kauli hiyo juzi kwenye mdahalo wa Katiba ulioandaliwa na Taasisi ya Vijana (TYVA), kwa kushirikiana na Kituo cha Televisheni cha EATV, Makumbusho ya Taifa, jijini Dar es Salaam.

Mwakilishi kutoka taasisi hiyo, Geofrey Mitande, alisema Katiba ya sasa inatoa nafasi kwa wabunge kukaa miaka mingi kwenye nafasi ya ubunge na kuziba wengine kuingia suala linalochangia kukosekana kwa mawazo mapya.

"Unakuta mbunge amekaa kwenye jimbo zaidi ya miaka 20, mwingine mpaka umri umekwenda, lakini anachaguliwa tu, sasa kwa hali hii siyo rahisi kupata mawazo mapya au kijana kupata nafasi. Inabidi ifike wakati hasa wakati huu wa mchakato wa kupata Katiba mpya, iweke ukomo katika nafasi hiyo," alisema Mitande.

"Tunahitaji Katiba, lakini sheria ambazo zitaisapoti hasa katika kumuinua kijana, kufanya hivyo kutasaidia vijana wengi kupata fursa ya kuingia kwenye siasa na kupata nafasi za ubunge tofauti na ilivyo sasa. Wengi wanaoingia ni wale wale na vijana ni wa kuhesabu hasa kwenye majimbo."

Magdalena Gise, alisema uwapo wa wabunge wale wale bungeni miaka yote kunachangia wawe na mazoea na kupitisha baadhi ya mambo ambayo hayana masilahi kwa wananchi wao.

"Unakuta wabunge ambao wemetumwa kwenda kuwawakilisha bungeni, hawafanyi kazi hiyo, wanashindwa kukaa na wananchi wao kufahamu matatizo na mahitaji yao, kwa sababu ya kushindwa kujiandaa wanaunga mkono kila kitu kinachowekwa mbele yao hata kama hakina manufaa kwa waliowatuma," alisema Gise.

"Tunahitaji Katiba mpya ndiyo itarekebisha haya yote, tunataka mawazo mapya kwenye nafasi za uongozi ikiwamo za kisiasa, tunataka kiongozi anapopewa kazi na wananchi ionekane kufanyika na siyo vinginevyo."

Gise alisema kilio chao kingine ambacho wanategemea Katiba mpya ilifanyie kazi ni kutaka viongozi kushtakiwa wanapofanya vibaya madaraka yao au kutumia vibaya nafasi zao.

"Ndiyo maana kule bungeni tuna viongozi wengi ambao wao kazi yao ni kunga mkono tu kila kitu hata kama ni kibaya.

Pia tunataka sheria ya kuwapa kinga viongozi pamoja na wabunge iondolewe ili wawe wanashtakiwa," alisema Gise.

Charles Mnepe, mshiriki katika mjadala huo, alisema wanaamini kwamba serikali ya awamu ya sita itasikia kilio cha wananchi na kuwapatia Katiba mpya kuleta matumaini kwenye maeneo mengi yanayolalamikiwa kwa sasa na tuna furaha kushirikiana na EATV katika mjadala huu."

# Kamati ya Bunge yataka tathmini misamaha kodi

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imetoa mapendekezo matatu kwa serikali, ikiwamo kufanya tathmini ya misamaha ya kodi inayotolewa ili kuona kama imeleta matokeo yaliyokusudiwa.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Daniel Sillo, alitoa mapendekezo hayo jana bungeni alipowasilisha maoni ya kamati hilo baada ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kusoma Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023 kwa mara ya pili na ya tatu.

Alisema tathmini hiyo itaisaidia serikali kujua ni kwa kiasi gani misamaha inayotolewa inachangia katika ukuaji wa uchumi na kama kuna haja ya misamaha hiyo kuendelea kuwapo, kuongezwa muda, kusitishwa au kuboreshwa.

Sillo alisema kamati pia inaishauri serikali kuhakikisha maboresho ya misingi ya utoaji haki katika usimamizi wa kodi ikiwa ni pamoja na kuweka muda wa upokeaji na utoaji wa marejesho ya mapingamizi ya kodi yaende sambamba na urejeshaji wa kodi kwa wakati pale tu uamuzi unapofanyika, ili kuwaondolea adha wafanyabiashara kusubiri marejesho kwa muda mrefu.

Aliitaka serikali kusimamia vyema utekelezaji wa kifungu cha 84 kifungu kidogo cha 3 kipengele A cha Sheria ya Kodi la Ongezeko ya Thamani (VAT), Sura 148 ambacho kinaelekeza marejesho yafanyike ndani ya siku 90.

Kuhusu uwasilishwaji wa muswada huo, kamati iliishauri serikali kuhakikisha unawasilishwa bungeni mapema walau mwezi mmoja kabla haujapitishwa na Bunge, ili wabunge wapate muda wa kutosha kuujadili.

"Muswada huu ni muhimu kwa maslahi ya Taifa na kwa mujibu wa Ibara ya 138 ya Katiba. Kamati inaishauri serikali kuhakikisha muswada unawasilishwa bungeni mapema zaidi walau mwezi mmoja kabla haujapitishwa na Bunge," alisema Daniel.

Awali, akisoma muswada huo kwa mara pili na ya tatu, Waziri Mwigulu alisema unakusudia kufanya marekebisho ya sheria 18 zinazohusu mfumo wa kodi, ikiwamo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali pamoja na taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya serikali. Bunge hilo lilipitisha muswada huo.


TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

i. Wananchi wote mnatangaziwa kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) utaondosha kwa njia ya mnada wa hadhara mali mbalimbali chakavu zilizokuwa zinatumika kwenye maaeneo ya Utekelezaji wa Mpango.
ii. Mali zitakazouzwa ni vifaa mbalimbali vya ofisi chakavu.
iii. Mnada huo utafanyika katika mikoa mbalimbali kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:

| Na | Mkoa na Mali zitakazouzwa | Tarehe | Mahali |
|---|---|---|---|
| 1 | Dar es salaam | 8th Julai 2023 | Ofisi za TASAF Tawi la Dar Es Salaam |
| 2 | Mwanza, Dodoma,Iringa Kigoma na Mbeya | 11 Julai 2023 | Ofisi ya Katibu Tawala |
| 3 | Pwani Tanga Manyara Kagera Tabora | 12 Julai 2023 | Ofisi ya Katibu Tawala |
| 4 | Rukwa, Arusha Njombe Mtwara Simiyu Ruvuma | 13 Julai 2023 | Ofisi ya Katibu Tawala |
| 5 | Morogoro Lindi Katavi Shinyanga Geita | 14 Julai 2023 | Ofisi ya Katibu Tawala |
| 6 | Songwe,,Pemba, Killimanjaro, Mara Singida | 18 Julai 2023 | Ofisi ya Katibu Tawala |

MASHARTI YA MNADA

i. kifaa kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo.
ii. Mnunuzi atalazimika kulipa asilimia mia moja (100%) ya thamani yote na kuondoa kifaa/vifaa atakavyonunua siku ya mnada.
iii. Ruhusa ya kuangalia vifaa itatolewa siku mbili (2) kabla ya terehe ya mnada.
iv. Mnada utaanza saa nne (4:00) Asubuhi katika kila kituo.

Mkurugenzi Mtendaji
Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – TASAF
Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete
S.L.P 2719 Dodoma ,Tanzania
simu: 255 026 2963866
Nukushi: 255 026 2963871
Barua pepe: info@tasaf.go.tz
Tovuti: www.tasaf.go.tzg

# Serikali yatoa hadhari ya simba wakazi Iringa wanaotembea usiku

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE tisa jana walisimama bungeni na kuhoji hatua zilizochukuliwa na serikali kudhibiti wanyamapori waharibifu.

Kukiwa na hoja hiyo, Wizara ya Maliasili na Utalii nayo ikataja mikakati na kutoa tahadhari kwa wakazi wa Iringa wasitembee usiku ili kuepuka kuvamiwa na simba waliotoka Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Katika kipindi cha 'Maswali' bungeni jana, Spika Tulia Ackson alilazimika kutoa nafasi kwa wabunge waliosimama kuuliza maswali ya nyongeza kutokana na swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Maimuna Pathan aliyetaka kujua mikakati ya serikali kudhibiti uvamizi wa tembo katika mashamba ya wilaya za Liwale na Nachingwea.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega alisema pamoja na tembo kuvamia maeneo mbalimbali, hivi karibuni katika kata zake mbili, simba walivamia mifugo ya wananchi na kuila, hivyo kusababisha taharuki kubwa.

Alihoji mkakati wa serikali kuhakikisha wananchi wanakua huru.

Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko, alisema wanyama wakali wakishadhuru binadamu, serikali inatoa kifuta jasho Sh. 500,000, akiuawa inatoa Sh. milioni moja, akihoji kwanini serikali isipitie upya kanuni zake ili kuja na uhalisia wa kutoa kifuta jasho kinachostahili.

Mbunge wa Kilolo (CCM), Justine Nyamoga, alisema Kata ya Ruaha Mbuyuni ina madhara makubwa yanayosababishwa na tembo, hali inayochangia upungufu wa chakula na kuhoji mkakati wa serikali kudhibiti tembo hao kwa kuongeza askari.

Mbunge wa Mwibara (CCM), Charles Kajege, alisema tatizo la tembo, mamba na kiboko ni kubwa katika jimbo hilo. Wameua wananchi na kuhoji mpango wa serikali kumaliza tatizo hilo.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema serikali inaangalia njia mbadala na kutatua migogoro ya wanyama wakali na waharibifu.

Alitaja njia za kuwadhibiti kuwa ni kujenga vituo, kuajiri askari wa vijiji (VGS) na kuweka fensi ya umeme katika baadhi ya maeneo ili kupunguza athari za wanyama hao wakali na waharibifu.

Mary pia alisema serikali iko katika mchakato wa kupitia upya sheria na kanuni zinazohusu malipo ya kiwango cha fidia zinazotokana na uharibifu wa wanyamapori yaongezwe.

Alisema fidia zinazolipwa kwa wanaoathirika na wanyama hao ni ndogo, haziendani na hali halisi ya sasa na kuhoji serikali haioni haja ya kuongeza kiwango cha fidia zinazotokana na uharibifu wa wanyamapori.

Kuhusu simba waliovamia Iringa, Naibu Waziri aliliambia Bunge kuwa kuwamekuwa na tatizo katika Mkoa wa Iringa la uvamizi wa simba katika baadhi ya maeneo.

"Ninaomba niwataarifu wananchi ninadhani wameona juhudi za serikali kutokana na uvamizi huu. Tangu utokee tumekuwa karibu na wananchi, tunatoa elimu na niendelee kutoa elimu kupitia Bunge hili kwamba wakati huu ambao tunasaka simba, wananchi wawe na tahadhari.

"Wanaotembea usiku, wenye mifugo... wawashe moto katika maeneo ya mifugo ili simba wasisogee katika maeneo hayo,"alisema.

Pia alisema wanaendelea kulinda maisha ya wananchi hasa wa mkoa huo na kwamba helikopta inaendelea kuzunguka kuwasaka samba hao ili wachukuliwe na kurudishwa katika maeneo yao.

Pamoja na hayo, Mary aliahidi kuwa serikali itaongeza nguvu ya askari ili kusaidia inapotokea dharura katika maeneo hayo.

Akijibu swali la msingi la Mbunge Maimuna, Naibu Waziri huyo alisema kwa sasa serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Wanyamapori Wakali na Waharibifu wa mwaka 2020-2024.

Alifafanua kuwa wizara inaendelea kutoa elimu juu ya kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu, kujenga vituo vya askari wanyamapori ili kusogeza huduma karibu na wananchi, kufunga mikanda tembo na kuanzisha timu maalum.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akimsikiliza mratibu wa ujenzi wa uwanja mpya wa Mashujaa, Meshach Bandawe (kulia), alipotembelea mradi huo unaojengwa katika Mji wa serikali Mtumba jijini Dodoma jana. Uwanja huo unatarajiwa kukamilika Juni 30. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Putin atoa neno uasi wa Wagner

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amesifu kampuni mbalimbali nchini humo kwa kuhakikisha uendeshaji thabiti wa sekta zao katika kukabiliana na changamoto kali za nje ya taifa hilo.

Kwa mujibu wa AFP, hiyo ni kauli ya kwanza kutolewa na Rais Putin tangu kutokea kwa uasi wa kundi la Wagner hivi karibuni, licha ya kwamba hakutaja mpango uliofanya Mkuu wa Wagner, Yevgeny Prigozhin kukubali kusimamisha askari wake na kuhamia Belarus.

Awali Putin alishutumu mamluki wa Wagner kwa uhaini na kuyataja matendo yao kuwa usaliti, huku ikielezwa kuwa ujumbe wa video uliotolewa na Rais Putin jana una maana kuwa shughuli zinaendelea kama kawaida kwa Kremlin.

Waziri Mkuu wa Russia, Mikhail Mishustin, alisema Russia imekabiliwa na changamoto kwa uthabiti wake na lazima ibaki na umoja nyuma ya Rais Putin.

Mishustin pia alisema chini ya uongozi wa Rais Putin, maofisa wa serikali walifanya kazi kwa umoja ili kuhakikisha utulivu baada ya uasi uliofanywa na Wagner.

"Jambo kuu katika hali hizi ni kuhakikisha uhuru wa nchi yetu, usalama na ustawi wa raia. Pia nitoe wito kwa Warussia kuendelea kusimama na Rais Putin," alisema.

Ilielezwa kuwa Waziri wa Ulinzi wa Russia, Sergey Shoigu, alionekana kupitia kipande cha video iliyotumwa na wizara hiyo akitembele wanajeshi wa taifa hilo walioko Ukraine baada ya uasi wa Wagner na hakukuonekana dalili za kujiuzulu baada ya Prigozhin kumtaka afanye hivyo.

Ilibainishwa kwamba kutolewa kwa video hiyo kulilenga kuonyesha hali ya utulivu baada ya mamluki wa Wagner kuuteka mji wa Rostov-on-Don na kuandamana bila kupingwa kuelekea Moscow.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa haijulikani nini kitatokea kwa Prigozhin na vikosi vyake licha ya kwamba mvutano kati ya mkuu wa mamluki na Jeshi la Russia umekuwa ukiongezeka kwa miezi kadhaa. **BBC**

MAUAJI DADA WA BILIONEA MSUYA

# 'Polisi walichukua dola kwa mshtakiwa'

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Revocatus Muyela anayetuhumiwa kumuua mdogo wa marehemu Erasto Msuya, maarufu Bilionea Msuya, Aneth Msuya, kupitia wakili wake amedai wakati anakamatwa na polisi, alikuwa na Dola za Marekani 450, Sh. 60,000 na simu tatu ambazo hadi leo hazijulikani zilipo.

Pia amedai kuwa vitu hivyo vilichukuliwa bila kufuata utaratibu na kwamba wakati anakamatwa, hakukutwa na nyaraka zake binafsi.

Muyela alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda Dar es Salaam, kupitia Wakili wake, Peter Kibatala kipindi anamuuliza maswali shahidi wa 14 wa upande wa Jamhuri, Inspekta Mahita Omary Mahita.

**Kibatala:** Mshtakiwa amenieleza kuwa wakati anakamatwa, alikuwa na simu zake tatu na anadai kuwa mlizichukua.

**Mahita:** Mimi sijui kuhusu simu

**Kibatala:** Yeye anasema ulipomkamata, ulimkuta na simu pamoja na dola za Marekani 450,000 na hadi leo hazijulikani zilipo

**Mahita:** Siyo kweli

**Kibatala:** Shahidi kwani ulishawahi kugombana na mshtakiwa?

**Mahita:** Sijawahi kugombana naye.

**Kibatala:** Kwanini yeye atunge sentensi kama hii?

**Mahita:** Sijui yeye.

**Kibatala:** Pia mshtakiwa amenieleza kwamba mlichukua Sh. 60,000 wakati mmemkamata bila kufuata utaratibu.

**Mahita:** Hajachukuliwa kitu chochote, hayo ni maneno yake tu.

**Kibatala:** Mshtakiwa pia anadai kuwa wewe ulichukua bastola yake.

**Mahita:** Sio kweli.

Wakati shahidi huyo, akiongozwa na Wakili wa Serikali, Generosa Montano kutoa ushahidi wake kabla ya Kibatala kumuuliza maswali, aliieleza mahakama jinsi alivyomkamata mshtakiwa huyo mkoani Arusha.

Alidai kuwa Agosti 19, 2016, akiwa na cheo cha Insepkta Msaidizi wa Polisi, alipata taarifa saa 10 jioni kuwa gari analotumia mshtakiwa Muyela limeonekana limepaki eneo la Mnara Mwene karibu na ofisi za CCM.

"Nikiwa na askari wangu wa doria tulikwenda hadi eneo hilo, kweli tukalikuta gari aina ya Range Rover toleo la kwanza, ambapo nilimjulisha afande RCO na mpelelezi wa kesi hiyo kuwa mshtakiwa anayetuhumiwa kwa mauaji yupo ndani ya gari.

"Baada ya taarifa hiyo, nilipewa maelekezo kwamba nitafute mbinu nzuri za kuweza kumkamata mshtakiwa. Mmoja wa askari ambao nilikuwa nao, Koplo Abdallah alikuwa anafahamiana na mtuhumiwa, nikamwambia aende amwombe lifti ampeleke hadi kituoni," alidai Mahita.

Alidai kuwa Koplo Abdallah alifanya hivyo na mshtakiwa alikubali kumpa lifti hadi Kituo Kikuu cha Polisi Arusha. Walipofika walimkuta kwa kuwa walitangulia kufika kituoni.

"Walishuka katika gari Koplo Abdallah na Muyela. Mimi nilijitambulisha kwake na yeye alijitambulisha kwangu ambapo nilimwelekeza kwamba yupo chini ya ulinzi kwa tuhuma za mauji aliyoyofanya Dar es Salaam na wapelelezi uko njiani, kwa hiyo awekwe mahabusu," alidai.

Mbali na Muyela, mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni mke wa aliyekuwa mfanyabiashara maarufu wa madini mkoani Arusha, marehemu Erasto Msuya, Miriam Mrita.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya wifi yake huyo Aneth aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada Kigamboni jijini Dar es Salaam, amekiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wenye ulemavu wapewe haki kama wengine kwenye ajira

**SUALA** la watu wenye ulemavu kulalamika kunyimwa haki katika mambo mbalimbali limekuwa likijitokeza mara kwa mara na kuwafanya wajisikie wanyonge.

Pia watu wenye ulemavu hutoa malalamiko kwa kukosa miundombinu rafiki katika baadhi ya majengo wanayokwenda kupata huduma muhimu na kusababisha wakose mahitaji wanayotaka.

Katika sehemu za huduma za kijamii kwa mfano kwenye baadhi ya kumbi za starehe, hoteli kunakosekana mazingira rafiki hasa wanapokwenda maliwatoni.

Katika kushughulikia tatizo la ajira, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, aliwakumbusha waajiri nchini kutoa nafasi kwa watu wenye ulemavu kupata mafunzo ya kuendeleza ujuzi katika maeneo ya kazi ili kutengeneza jamii ya ujuzi na ujumuishwaji kwa watu wote.

Akifungua mkutano mkuu wa 64 wa wanachama wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), uliofanyika mwishoni mwa wiki Dar es Salaam.

Ushauri wa waziri ni kuhakikisha programu za kukuza ujuzi zinakuwa endelevu, serikali ilipendekeza kupunguza tozo ya kuendeleza ujuzi kutoka asilimia nne hadi 3.5 na kuahidi kuendelea kuipunguza ili kuwapunguzia mzigo waajiri na kuchochea fursa za ajira nchini.

Pia Waziri wa Fedha amependekeza kuwa sehemu ya makusanyo ya tozo ya kuendeleza ujuzi, itengwe chini ya wizara inayojishughulisha na masuala ya ajira kwa lengo la kuendeleza programu ya mafunzo sehemu za kazi.

Ushauri wa serikali ni kuwataka waajiri ambao bado hawajajiunga na chama hicho, kufanya hivyo ili kuongeza nguvu ya kuwa na sauti ya pamoja na namna ya kurahisisha kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza.

ATE pia imepongezwa kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika masuala mbalimbali ikiwamo ya kuhamasisha usawa wa kijinsia katika maeneo ya kazi hasa kupitia utekelezaji wa programu ya mwanamke kiongozi inayolenga kuwajengea uwezo wanawake kushika nafasi za juu za uongozi, kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali katika maeneo ya kazi, kuwa mstari wa mbele pia katika masuala ya afya na asalama mahala pa kazi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzane Doran, alisema kupitia programu ya mafunzo ya taifa ya kukuza ujuzi, serikali imetoa fursa ya mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri au kuajiriwa kwa vijana 14,542 kupitia mafunzo ya uanagenzi na uzoefu kazini.

Hii ni fursa nzuri kwa vijana wote bila kujali jinsia zao kuitumia ili kujiongezea ujuzi na kuwawezesha kupata ajira kwa urahisi.

Ofisa Mtendaji huyo anakumbusha kuwa mkutano wa mwaka huu unalenga kuchochea ushiriki wa wadau wa kisekta, wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi na vyuo vya elimu ya ufundi na sekali kwa ujumla katika sekta kuu za uchumi.

Badala ya vijana kuendelea kulalamikia ukosefu wa ajira ni vizuri wakatumia fursa hiyo ya mafunzo ili kujiongezea ujuzi na maarifa ambayo yatawasaidia kujiajiri wenyewe badala ya kusubiri ajira zinazotolea na serikali.

Wengi wa vijana wameamua kujiingiza katika fani za ujasiriamali baada ya kuona ajira zinakuwa ngumu kupatikana na hiyo imetokana na wao kupata uzoefu wa kujiendeshea shughuli zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Shule zinapoanza mazingira yaboreshwe

**WANAFUNZI** wanaporejea shuleni wiki ijayo Jumatatu Julai 3, wazazi na walezi wanazitazama mamlaka zinazohusika na kusimamia elimu iwapo zimetengeneza mazingira ya kusoma na kufundishwa yaliyo bora zaidi kuliko watoto walivyoyaacha.

Ni kero kuona watoto wakipanga foleni, kujisaidia sababu ya tatizo sugu la upungufu wa matundu ya vyoo shuleni lakini wengine wakilazimika kujibanza kwenye vichaka, mashamba ya watu au vyoo vya majirani na shule na kwenye bustani za maua wanaposhikwa na haja.

Tukumbuke kero ya kukosa vyoo na maji inawaumiza zaidi wanafunzi wa kike ambao pamoja na kuhitaji huduma za choo kama walivyo wengine wana mahitaji ya kijinsia ambayo ni muhimu kuzingatiwa na changamoto hiyo kutatuliwa kuondoa utoro na kuwafanya kuchukia siku zao kwa vile inakuwa kama zinawaletea aibu na kukosa amani.

Wasichana 25 wanapaswa kutumia tundu moja la choo wakati wavulana ni 20 kwa tundu moja, ni kwa mujibu wa Sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 inayoelekeza hayo, licha ya kwamba wasichana pia wanahitaji kuwa na chumba maalumu cha kubadilisha na kuhifadhi taka za pedi.

Ikumbukwe kukosekana vyoo shuleni kunaathiri wanafunzi kijinsia kwani badala ya kufikiria masomo wapo wanaowaza jinsi ya kukimbia na kuwahi chooni unapofika wakati wa mapunziko, ili kukwepa foleni au misururu ya kuingia chooni. Wengine wanafikiria kero ya harufu mbaya vyooni, lakini pia wapo wanaochoshwa na mazingira mabovu ya kujifunzia na kuichukia shule.

Mazingira salama shuleni yanaanza na kuwapo vyoo bila choo kuna hatari nyingi za maradhi kama kuzagaa kinyesi na mkono kwenye viwanja vya shule, harufu mbaya kutoka maliwatoni, inzi kuzagaa na kusambaza maradhi lakini wasichana kuathirika kwa vile watalazimika kukosa masomo kutokana na taratibu za maumbile za kila mwezi.

Wakati umefika kwa wazazi na walezi pamoja na viongozi wa kisiasa wa maeneo zilizoko shule za umma kuona na kuanza kutatua matatizo ya mahali wanakosoma watoto wao mapema kabla mambo hayajawa mabaya mfano kuamua kuchimba mashimo ya vyoo kwa kutumia nguvu za wananchi.

Aidha, kuboresha miundombinu kwa kuipa sura ya usasa zaidi mfano kushirikiana kununua sementi na kujenga kama vyoo vimebomoka. Kama ni eneo lenye maji karibu kuvuta maji hadi kwenye vyoo vya shule au hata kununua mapipa au kujenga visima vya kuhifadhi maji ya mvua au kujaza maji kwa magari ili kuwasaidia watoto wasome eneo salama, wakichangishana wenyeji kisha kuomba nguvu ya serikali.

Ni vyema pia kuweka upya milango ambayo imebomoka, hili ni suala la kupewa kipaumbele kwa vile shule nyingi zina vyoo visivyo na milango wazazi waonae namna bora ya kutengeneza milango na kuweka mazingira bora ya kusoma na kufundisha watoto wao.

Lakini pamoja na juhudi za wazazi na walezi viongozi wa wilaya washirikiane na wadau kuboresha miundombinu ya elimu kwa wanafunzi na kusoma katika mazingira rafiki.

Wakumbuke mwanafunzi akisoma katika mazingira rafiki ufaulu wake unakuwa bora lakini wakiachwa kusoma kwenye shule ambazo hazina madawati wanakalia viroba, hakuna choo wanajisaidia mashambani na kwenye bustani za maua ufaulu unaweza kutetereka.

Tanzania ni kubwa wapo baadhi ya watu wamesoma kwenye shule za vijijini au mijini maeneo walikozaliwa, leo wana nafasi ikiwa ni pamoja kufanikiwa kibiashara, kikazi au kisiasa hawa nao wana mchango kuhakikisha kuwa wanaboresha mazingira ya kusoma.

Wanaweza kufanikisha juhudi hizo kwa kutumia ushawishi walionao kisiasa au kwenye nafasi za uongozi. Lakini wanaweza kutumia faida za biashara zao kusaidia wengine kwenye maeneo wanapoishi na waliposoma.

Shime watoto wetu wanapofungua shule wakute miundombinu salama na mazingira tulivu ya kimasomo, ili wanafunzi wasome katika mazingira rafiki lakini waone juhudi za kusaidia kuboresha shule zao.

# Waajiri watakiwa kutoa nafasi ajira wenye ulemavu

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amewataka waajiri nchini kutoa nafasi kwa watu wenye ulemavu kupata mafunzo ya kuendeleza ujuzi katika maeneo ya kazi ili kutengeneza jamii ya ujuzi na ujumuishwaji kwa watu wote.

Katambi alitoa kauli hiyo wakati akifungua mkutano mkuu wa 64 wa wanachama wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), uliofanyika mwishoni mwa wiki Dar es Salaam.

"Katika kuhakikisha programu za kukuza ujuzi zinakuwa endelevu, serikali ilipendekeza kupunguza tozo ya kuendeleza ujuzi kutoka asilimia nne hadi 3.5 na kuahidi kuendelea kuipunguza ili kuwapunguzia mzigo waajiri na kuchochea fursa za ajira nchini," alisema Katambi.

"Pia Waziri wa Fedha amependekeza kuwa sehemu ya makusanyo ya tozo ya kuendeleza ujuzi, itengwe chini ya wizara inayojishughulisha na masuala ya ajira kwa lengo la kuendeleza programu ya mafunzo sehemu za kazi."

Katambi alisema ipo haja kwa waajiri ambao bado hawajajiunga na chama hicho, kufanya hivyo ili kuongeza nguvu ya kuwa na sauti ya pamoja na namna ya kurahisisha kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza.

"Niendelee kuwapongeza ATE kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika masuala mbalimbali ikiwamo ya kuhamasisha usawa wa kijinsia katika maeneo ya kazi hasa kupitia utekelezaji wa programu ya mwanamke kiongozi inayolenga kuwajengea uwezo wanawake kushika nafasi za juu za uongozi, kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali katika maeneo ya kazi, kuwa mstari wa mbele pia katika masuala ya afya na usalama mahala pa kazi," alisema Katambi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzane Doran, alisema kupitia programu ya mafunzo ya taifa ya kukuza ujuzi, serikali imetoa fursa ya mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri au kuajiriwa kwa vijana 14,542 kupitia mafunzo ya uanagenzi na uzoefu kazini.

Alisema mkutano wa mwaka huu unalenga kuchochea ushiriki wa wadau wa kisekta, wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi na vyuo vya elimu ya ufundi na serikali kwa ujumla katika sekta kuu za uchumi.



Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, Seleman Bishagazi (kushoto), akitoa elimu ya jinsi ya kuzuia ukatili wa kijinsia kwa wanachama wa UWT wa Wilaya ya Ilala jana, iliambatana na mafunzo ya ujasiriamali, ukiwamo wa kutengeneza mkaa mbadala. **PICHA: SABATO KASIKA**

# BAKWATA, halmashauri wavutana eneo la stendi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Mwanza limeitaka Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuacha kufanya shughuli zake katika eneo la stendi ndogo ya Igombe, iliyopo katika barabara ya Kenyatta Kata ya Pamba mkoani humo, baada ya kutoa siku 14 za mazungumzo ambayo yalishindikana kufanyika.

Aidha, imeelezwa kuwa eneo hilo linalomilikiwa na BAKWATA lilichukuliwa kinyume cha sheria na halmashauri hiyo ambayo iliendeleza shughuli zake, ikiwa ni pamoja na kupangisha wafanyabiashara na kutumia eneo hilo kama stendi ndogo.

Akizungumza na Nipashe kufuatia mgogoro huo ambao umedumu kwa muda mrefu, Shekh wa Mkoa wa Mwanza, Hasani Kabeke, alisema uamuzi wa mahakama ulitoka Juni 3, 2020, lakini halmashauri hiyo iligoma kuachia eneo hilo.

Alieleza kuwa baada ya Juni 3, 2020 baraza hilo kushinda kesi baina yao na jiji juu ya umiliki wa kiwanja hicho ambacho kinatumiwa na halmashauri kama stendi na kuendelea kukusanya ushuru katika eneo hilo waliamua kuikazia hukumu ili kupata ufafanuzi zaidi.

Aliendelea kusema mahakama ilitoa ufafanuzi Juni 3, 2022 kuwa halmashauri inatakiwa kufanya jambo moja kati ya mambo mawili ambayo ni aidha kurudisha kiwanja hicho katika umiliki wa BAKWATA au kuwalipa Sh. milioni 539 kwa baraza hilo na kupewa muda wa siku 90 kutekeleza amri hiyo.

Alieleza kuwa licha ya amri hiyo jiji walikaidi kufanya hivyo ambako baraza hilo liliweka juhudi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuwatumia barua mara kadhaa bila mafanikio pamoja na kukutana na viongozi mbalimbali akiwamo meya, mkurugenzi pamoja na mwanasheria, lakini hakukuwa na utekelezaji wa amri hiyo ya Mahakama.

"Ilibidi Juni 7, tuchukue hatua ya kuenda katika eneo hilo la stendi kwa ajili ya kufanya dua ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kushinda kesi hiyo na kuishukuru mahakama kwa kuendelea kutenda haki ndani ya nchi yetu," alibainisha.

Aidha, alieleza kuwa baada ya dua hiyo walitoa wiki mbili kwa halmashauri na kuwataka kukutana na baraza hilo ili wazungumze na endapo wakishindwa kutimiza hilo watawaita wawekezaji wengine ili kuwekeza mradi wowote katika eneo hilo.

"Milango ya jiji katika hilo la uwekezaji bado haijafungwa, lakini hiyo Sh. milioni 539 hatuitaki tena kwani muda uliotolewa na mahakama umekwisha na bado fedha hiyo haiendani na soko ikumbukwe hata jiji wenyewe ni juzi tu waliuza viwanja kwa Shilingi bilioni moja kwa kila kimoja," alisema.

Aliendelea kusema kuwa baada ya hizo wiki mbili wataangalia watu walileta maombi na ifikapo Julai 8, 2023 watatoa taarifa rasmi ya mwendelezo wa kiwanja hicho ambayo itatolewa katika eneo hilo la stendi.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wote katika eneo hilo kuacha kulipia kodi katika halmashari na kuonana na uongozi wa BAKWATA ili kupewa utaratibu wa malipo huku akisisitiza kuwa eneo hilo siyo la jiji bali ni la Baraza hilo na kusema kuwa kwa watakaoendelea kulipa katika halmashauri watakuwa wakiingia hasara.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu Meya wa Halmashuri ya Jiji la Mwanza, Sima Constantine Sima, alithibitisha kuwapo kwa tatizo ambako alisema kama halmashauri walishakaa na baraza hilo na kuelewana juu ya mstakhabari wa eneo hilo, lakini baada ya muda Mkurugenzi aliyekuwapo akawa ameondolewa na wanasubiri mkurugenzi aliyeteuliwa akija Julai 3, 2023 watakaa tena ili kumaliza suala hilo.

Aidha, alithibitisha kuwa halmashauri hawakulitendea haki Baraza hilo baada ya kushinda kesi, kwa kuwa hawakutakiwa kukaa kimya kwa muda wote huo kutokana na ukaribu uliopo baina yao na serikali.

Stendi hiyo maarufu kama stendi ya Igombe ni stendi pekee iliyopo katikati ya Jiji la Mwanza kwa ajili ya daladala zinazotoka maeneo ya Airport, Ilemela, Buswelu pamoja na maeneo mengine ya Mwanza zikielekea Buhongwa, Nyanshishi, Usagara, Butimba na stendi kuu ya mabasi Nyegezi na Baraza hilo limeahidi kuifanyia shughuli nyingine kama halmashauri itashindwa kufika makubaliano.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



**TANGAZO**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz


NFRA

# TANGAZO KWA UMMA

## VITUO VYA UNUNUZI WA AKIBA YA CHAKULA YA TAIFA KWA MSIMU WA 2023/2024

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua, kuhifadhi na kuzungusha akiba ya chakula ili kukabiliana na upungufu wa chakula na majanga mengine ya Kitaifa yanayoweza kujitokeza. NFRA hununua nafaka kila mwaka kwa ajili ya akiba ya chakula ya Taifa. Kwa msimu huu wa mavuno ununuzi umeanza rasmi tarehe 22 Juni, 2023.

Wakala unategemea kutumia vituo kwenye mikoa mbalimbali, ambavyo vitakua vinafunguliwa kwa kuangalia hali ya ukaukaji wa nafaka, uzalishaji wa ziada wa zao husika (mahindi na mpunga), eneo kuwa na ghala zuri la kuhifadhia nafaka, bei ya soko, usalama wa eneo, mgawanyiko wa kijiografia na kuwepo na huduma muhimu.

Kwa kuanzia, NFRA itafungua vituo vya ununuzi wa mahindi kwenye kanda zifuatazo zenye uzalishaji na upatikanaji mkubwa wa nafaka; Songea (Mkoa ya Ruvuma), Makambako (Mikoa wa Njombe na Iringa), Songwe (Mikoa wa Songwe na Mbeya), Sumbawanga (Mikoa ya Rukwa na Katavi), Dodoma (Dodoma na Manyoni), Arusha (Arusha na Manyara) na Shinyanga (Mkoa wa Kigoma na Tabora). Aidha, mpunga utanunuliwa katika Mikoa ya Iringa, Morogoro, Songwe, Mbeya na Tabora.

**MCHANGANUO WA VITUO VYA UNUNUZI WA NAFAKA NA BEI KWA MSIMU WA 2023/2024**

| Na. | KANDA | MKOA | WILAYA | KITUO | BEI (TZS) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | MAHINDI | MPUNGA |
| 1 | ARUSHA | Arusha | Karatu | Karatu | 900-1,000 | |
| | | Manyara | Babati | Babati | | |
| 2 | DODOMA | Dodoma | Dodoma Mjini | Kizota (Ghala kuu) | 700-800 | |
| | | Manyara | Kiteto | Kiteto | | |
| 3 | KIPAWA | Morogoro | Mvomero | Mvomero | | |
| | | Tanga | Handeni | Handeni | 800 | |
| 4 | MAKAMBAKO | Iringa | Kilolo | Ilula | 700-800 | 900-1,000 |
| | | | Iringa Vijijini | Pawaga | | |
| | | Njombe | Ludewa | Mlangali | | |
| | | | | Shaurimoyo | | |
| | | | Njombe DC | Makambako (Ghala Kuu) | | |
| | | | Wanging'ombe | Igula | | |
| | | Mbeya | Mbalali | Uturo | | |
| | | | | Madibira | | |
| | | | | Chimala | | |
| 5 | SHINYANGA | Shinyanga | Shinyanga Mjini | Shinyanga (Ghala kuu) | 750-950 | 900-1,000 |
| | | Tabora | Nzega | Bukene | | |
| | | Kigoma | Kasulu | Mvugwe | | |
| 6 | SONGEA | Ruvuma | Songea Mjini | Ruhuwiko (Ghala Kuu) | 650-700 | |
| | | | Songea Vijijini | Magagura | | |
| | | | | Mgazini | | |
| | | | Madaba Mji | Madaba | | |
| | | | Mbinga | Mbinga | | |
| | | | Namtumbo | Namtumbo | | |
| | | | Nyasa | Tingi | | |
| | | | Tunduru | Tunduru | | |
| 7 | SONGWE | Songwe | Mbozi | Vwawa (Ghala Kuu) | 650-800 | 900-1,000 |
| | | | Ileje | Isongole | | |
| | | | Momba | Kakozi | | |
| | | | Momba | Nkala | | |
| | | | Momba | Chitete | | |
| | | | Momba | Naming'ong'o | | |
| | | Mbeya | Mbeya Vijijini | Inyala | 700-800 | 900-1,000 |
| | | | Kyela | Makwale | | |
| | | | Kyela | Ngana | | |
| 8 | SUMBAWANGA | Rukwa | Sumbawanga mjini | Mazwi (Ghala Kuu) | 600-800 | |
| | | | Sumbawanga vijijini | Laela | | |
| | | | | Mtowisa | | |
| | | | Kalambo | Mwimbi | | |
| | | | Nkasi | Namanyere | | |
| | | Katavi | Mpimbwe | Majimoto | 600-800 | |
| | | | Mlele | Kibaoni | | |
| | | | Tanganyika | Sibwesa | | |
| | | | | Kasekese | | |

**Utaratibu wa Ununuzi:**
Nafaka zote zitakazofikishwa katika vituo vya NFRA, zitapokelewa iwapo zitakidhi vigezo vya ubora kama vitakavyobainishwa kupitia Kanda za NFRA. Bei elekezi zitakazotumika zitapangwa kwa kuzingatia umbali kutoka ghala kuu la NFRA na bei za soko katika eneo husika. Utaratibu wa ununuzi wa nafaka kupitia Vyama vya Ushirika/Vikundi vya Wakulima, Wafanyabiashara na Mawakala utafanyika kupitia makubaliano yatakayofikiwa baina ya makundi hayo na Kanda za NFRA.

**Utaratibu wa Malipo:**
Malipo yote yatafanyika ndani ya siku tatu baada ya kukamilisha taratibu za kupokea nafaka.

Kwa maelezo zaidi kuhusu vituo vya ununuzi, utaratibu wa ununuzi na bei katika vituo husika, wasiliana na Meneja wa Kanda/Vituo vya NFRA vilivyo karibu yako.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**
**20 Juni, 2023.**

## Wajasiriamali wapewa mbinu kukuza uchumi, kipato

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SERIKALI imewapa mbinu wajasiriamali wadogo wa Wilaya ya Tanga namna ya kukuza uchumi, ikiwataka kutumia zaidi fursa ya maonyesho ya biashara kutangaza bidhaa zao.

Mkuu wa wilaya hiyo, Hashim Mgandilwa alisema fursa ya kujitangaza kupitia maonyesho ndiyo jukwaa mahususi lenye nguvu duniani kote kujitangaza, badala ya kufikiria kuuza pekee bidhaa zao.

Mgandilwa, alitoa mbinu hizo jana kwa wajasiriamali hao wa jijini Tanga, wakati akizindua msimu wa sita wa Tanga Women Gala.

Mgandilwa alisema baadhi ya wajasiriamali wamekuwa wakifika kwenye maonyesho wanaweka malengo ya kuuza mzigo walionao kwa siku hizo pekee, lakini wakimaliza hawahesabu faida wamepataje na mwisho wa siku wanaendelea na maisha.

Kutokana na udhaifu huo, aliwataka wabadilike na kuondokana na hali hiyo badala yake watumie kama jukwaa la kutafuta masoko muda wote kwa kujikita kutangaza biashara zao na siyo kuuza tu wakati wa maonyesho.

Alisema kwamba ni matumaini yake kwamba katika msimu huo wa sita wa Tanga Women wajasiriamali tunakwenda kutengeneza historia kubwa ambayo itakuwa chachu ya kuendelea kuwainua wajasiriamali mkoani humo kukua kiuchumi.

"Niwashukuru Tanga Women Gala kwa kazi kubwa mnaoendelea kuifanya tunajua inawezekana wakawa hawana cha kuwalipa lakini dua za wajasiriamali ambao kila siku mnaendelea kuwainua ndiyo malipo yenu," alisema.

Aidha, aliwataka kuendelea kupanua wigo kwa wajasiriamali ambao kimsingi hawana uwezo wa kufika kwenye maeneo yao kwa kutengeneza utaratibu wa namna ya kuweza kuwafikia na kuwatambua ili kuona namna ya kuwasaidia.

Awali, Mkurugenzi wa Kampuni ya Five Bothers Entertainment, Nasoro Makau, alisema tamasha hilo la Tanga Women Gala la msimu wa sita linatarajiwa kuwa la aina yake kutokana na namna walivyojipanga.

Naibu Meya wa Jiji la Tanga, Wakili Mwanaidi Kombo, akizungumza na wajasiriamali hao alitoa wito kwa wanawake kuendelea kuchangamkia fursa mbalimbali zilizopo ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Alisema: "Wakati tukichangamkia fursa hizo tusisahau majukumu mengine kama mwanamke changamoto nyingi za ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanafunzi kwa sababu sisi kinamama tumejikita kutafuta fedha badala ya majukumu yetu ya ndani."

# Tembo wafungwa visukuma mawimbi kudhibiti uharibifu

**Na Godfrey Mushi,** SAME

TAASISI ya Tanzania Elephant Foundation (TEF), kwa kushirikiana na serikali wameanza kuchukua hatua za kimkakati za udhibiti wanyamapori kuvamia makazi ya watu, kuharibu mazao na mali katika Wilaya za Same na Mwanga mkoani Kilimanjaro.

Udhibiti huo umefanyika kwa kuwafunga tembo wa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, visukuma mawimbi maarufu GPS Call's kwa ajili ya kufuatilia mienendo yao.

Vifaa hivyo maalum vya mawasiliano, ambavyo vimefungwa juu ya shingo za tembo wanne mpaka sasa, vinasaidia kutambua mienendo ya tembo hao hasa wale wanaotoroka hifadhini na kwenda kwenye jamii na kusababisha uharibifu kama kudhuru watu, uharibifu wa mazao na kuua watu.

Akizungumza jana na Nipashe katika mahojiano maalum kuhusiana na mradi huo, Mkurugenzi wa TEF, Lameck Mkuburo, alisema visukuma mawimbi hivyo, vina uwezo mkubwa wa kufuatilia mienendo yao na kuwadhibiti tembo, kabla ya kuleta madhara kwa wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo.

"TEF inajihusisha na uhifadhi wa tembo kupitia utafiti wa kisayansi, na kusaidia jamii kutatua migogoro kati ya binadamu na tembo katika jamii zinazozunguka hifadhi za taifa. Kwa sasa tuna miradi katika maeneo kuzunguka Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na ndani ya hifadhi katika kusaidia jamii kukabiliana na hizo changamoto zinazosababishwa na tembo.

"Vifaa hivi vinasaidia sana kutoa taarifa za papo kwa papo, ambazo zinaisaidia serikali na mamlaka nyingine za uhifadhi, kuchukua hatua za haraka kusaidia wananchi na kuwaondoa tembo kwenye maeneo ya makazi ya watu. Mpaka sasa hivi tembo wanne tumeshavalisha vifaa hivyo, lakini lengo ni kuvalisha tembo wanane.

Zaidi aliongeza, "Zoezi tumeliahirisha kwa muda kutokana na changamoto mbalimbali, lakini mwanzoni mwa Julai mwaka huu tutakwenda kumalizia tembo wengine wane," alisema Mkuburo.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Emanuel Moirana, akizungumzia vifaa hivyo, alisema kutekelezwa kwa mradi huo kutaongeza ufanisi na mpango wa serikali wa kukabiliana na migogoro baina ya tembo na binadamu, ambayo imekuwa tishio kwa wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo.

Kabla ya utekelezaji wa zoezi hilo la kufunga tembo visukuma mawimbi, Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Edward Kohi, alisema mradi huo utasaidia kuondoa madhara ya uharibifu wa mazao kwenye mashamba ya wakulima.

Kwa mujibu wa Dk. Kohi, makundi yote ya tembo yaliyoko ndani na nje ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, yatafungwa vifaa hivyo ambavyo huwezesha maofisa wanyamapori kuwafuatilia na kuwarudisha ndani ya hifadhi, kabla ya kuleta madhara kwenye makazi ya wananchi.



Mwanasheria wa Shirika lisilo la Kiserikali la Civil Social Protection Foundation (CSP), Eliakim Paulo (kulia), akizungumza kwenye warsha ya mradi wa tanzanite kwa uchumi imara wa mwanamke uliowahusisha wajasiriamali wanawake, wasaidizi wa kisheria na waandishi wa habari katika Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kiongozi mbio za Mwenge akoshwa utekelezaji miradi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MIRADI saba ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.628 imeipa 'heshima' Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, baada ya kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Abdalla Shaib Kaim, kueleza namna alivyofurahishwa na miradi inavyoibuliwa na kugusa mahitaji ya jamii husika, huku viwango vyake vikiwa havina mashaka.

Kaim aliyasema hayo jana baada ya kukagua na kuzindua Barabara ya Nyerere, yenye urefu wa kilomita 0.79 iliyojengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Sh. milioni 429.3 katika Kata ya Bomang'ombe, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai.

"Ninyi mnahitaji pongezi kwa viwango vilivyofanyika katika miradi yenu na hasa barabara hizi mnazojenga kwa kiwango cha lami. Hata kama lengo ni kurahisisha usafiri na usafirishaji, nataka wengine waje wajifunze kwenu maana hii ni alama ya mafanikio yenye tija kiuchumi," alisema kiongozi huyo.

Ukiwa wilayani Hai, Mwenge huo pia umezindua mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Shiri Njoro, iliyojengwa kwa gharama ya Sh. milioni 88 ili kuboresha na kusogeza karibu huduma za afya kwa wananchi wa vijiji vya Kata ya Mnadani.

Aidha, Mwenge huo umezindua mradi wa ujenzi wa tangi la maji eneo la Kilimambogo, Kata ya Bondeni, lililojengwa kwa Sh. milioni 100.


Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Amir Mkalipa, mradi huo unalenga kutatua kero ya majisafi na salama kwa wakazi 9,500 wa vijiji vya Kawaya, Rundugai, Chekimaji, Kilimambogo na Chemka.

Mingine ni mradi wa uhifadhi wa chanzo cha maji cha Njoro ya Blue-Rundugai, uliotumia zaidi ya Sh. milioni 15.8 kuhifadhi mazingira na kuwezesha kilimo cha umwagiliaji.

Pia upo mradi wa uoteshaji mboga na matunda unaotekelezwa na kikundi cha Youth Green Movement ulioko Kingereka B, Kata ya Bondeni ambao umrtumia Sh. milioni 31.

Vilevile, Mwenge huo umeweka jiwe la msingi ujenzi wa majengo manne na njia za wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Hai. Mradi uliojengwa kwa Sh. milioni 900, unalenga kuboresha, kusogeza huduma za afya kwa wananchi.

Kadhalika, ulizindua mradi wa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Sekondari Hai, ambao umegharimu Sh. milioni 64.2.



# Mashauri ya kinidhamu 99 yafanyiwa kazi Mahakama Kuu

**Na Halima Ikunji,** TABORA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Hamisi Juma ambaye ni Mwenyekiti wa Tume ya Mahakama na Utumishi amesema katika kipindi cha miaka saba wamepokea mashauri 99 ya kinidhamu dhidi ya watumishi na kufanikiwa kushughulikiwa na tume hiyo.

Alibainisha hayo juzi katika mkutano wa wadau uliowashirikisha viongozi mbalimbali wa serikali mkoani humo na kusema kuwa katika kipindi cha Desemba 2015 hadi Desemba 2022 tume hiyo ilipokea idadi hiyo ya mashauri yanayowahusu mahakimu kwenye masuala ya nidhamu kutoka katika kamati mbalimbali.

Alieleza kuwa asilimia 33 ya watumishi hao walifukuzwa kazi, kati ya hao asilimia 38 walisimamishwa kwa manufaa ya umma, asilimia 13 walipewa onyo na asilimia 15 walirudishwa kazini baada ya uchunguzi.

Prof. Ibrahimu alisema kwamba takwimu hizo zinaonesha kazi zilizokuwa zikifanywa na kamati hizo katika kuisaidia tume kuweza kutoa maamuzi yake na kuwa viongozi wa kamati hizo za maadili wanasaidia kuiheshimisha Mahakama.

Kuhusu mkoani Tabora alisema kutokana na mkoa huo kuwa mkubwa kadhalika na majukumu ya kiutendaji katika utoaji haki yamekuwa yakiongezeka na kusababisha kuwa mazito zaidi.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Dk. John Mboya, alisema kuwa kamati zote zinaendelea kutoa huduma kwa wananchi japokuwa wananchi hawajaelewa umuhimu uliopo.

Dk. Mboya alisema kwamba kupitia mkutano huo kamati zimepata elimu ya kutosha kuhusu namna bora ya kupokea malalamiko yaliyowasilishwa na wananchi kupitia kwa mtaala wa sheria.

# RC ataja sababu 5 hoja za CAG kukosa majibu H/shauri Msalala

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amebainisha sababu tano ambazo zinazosababisha hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kukosa majibu katika Halmashauri ya Msalala.

Halmashauri hiyo ilikuwa na hoja 59 kati ya hizo hoja 28 zilitatuliwa kwa kutafutiwa majibu na hoja 31 bado zinaendelea kushughulikiwa, hivyo bila kupata vielelezo vinavyohitaji hoja hizo zitaendelea kukosa majibu kila mwaka wa fedha.

Mndeme aliyabainisha hayo jana kwenye mkutano maalum wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Msalala lililokuwa na kazi ya kupitia na kujadili taarifa ya CAG.

Alisema moja ya sababu inayosababisha kuwapo kwa hoja hizo ni ukosefu wa hati miliki kwa maeneo yaliyotumika kujenga majengo ya halmashauri.

Alisema, sababu ya pili ni makusanyo ya mapato ya ndani kiasi cha Sh. milioni 214.5 yaliyokusanywa kwa mashine za posi hayakupelekwa benki kwa wakati na kusababisha kuibuka kwa hofu ya fedha hizo na kushindwa kuwa na taarifa sahihi kwanini hazikupelekwa benki.

Mndeme alisema kuwa hoja ya tatu ni ushuru wa huduma wa Sh. milioni 182.3 zilizokusanywa kutoka katika kampuni mbalimbali pasipokuwa na uthibitisho wa jumla ya makusanyo ya kampuni hizo kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambacho ni msingi wa kupata kilichokusanywa kwa mwaka husika wa fedha. Aidha, alisema sababu ya nne ni uwepo wa malipo ya Sh. milioni 144.13 zilizotolewa katika akaunti ya AMANA, yametekeleza shughuli tofauti na fedha hizo hazikuwa na kibali cha kamati ya fedha na nyingine ilikuwa kununua vifaa vya ujenzi vya Sh. milioni 39.7 kwa wazabuni ambao hawajasajiliwa.

Hata hivyo aliwashauri kuzingatia sheria na miongozi ya matumizi ya fedha za umma, taratibu za manunuzi na kufanya malipo kwa wazabuni ambao wanatambulika kisheria ili kuondoa hoja hizo ambazo zinatakiwa kuwa na majibu sahihi kila mwaka ili kuendelea kupata hati safi.

Mdhibiti na Mkaguzi wa Nje Mkoa wa Shinyanga, Patrick Lugisi, aliwataka kuwa na utaratibu wa wanashughulikia hoja hizo, wanapokwama watoe taarifa ili kuwapatia mwongozi wasije kujibu vitu ambavyo havihitajiki kwa sababu hoja hizo zinajibika pale watakapotafuta vielelezo sahihi.

Makamu Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Flora Sagasaga, alimtaka mkurugenzi kwa kushirikiana na idara ya ardhi na mipango miji kuhakikisha wanapima maeneo yote yaliyojengwa ofisi za umma na kuyakatia hati miliki ili kupunguza hoja za CAG ambazo kila mwaka zinazidi kuongezeka badala ya kupungua.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Hamisi Katimba alisema, moja ya kazi aliyopewa ni kuhakikisha anasimamia ukusanyaji wa mapato na kukamilisha miradi ya iliyoanzishwa katika sekta ya elimu, afya, maji, kilimo na miundombinu ya barabara na mpaka sasa halmashauri hiyo imeshakusanya mapato ya ndani kwa asilimia 103.



Mtaalamu wa mchakato wa kufunga migodi wa Barrick Buzwagi, Zonnastraal Mumbi, akifungua hafla ya wafanyakazi wanawake wa mgodi huo kwa ajili ya kuwapongeza na kuwatia moyo iliyofanyika mjini Kahama mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askofu: Watoto wazuiwe kuangalia tamthilia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ASKOFU wa Kanisa la International Evangelical Assemblies of God Tanzania (IEAGT) Kambi ya Waebrania Manispaa ya Shinyanga, David Mabushi, amewataka wazazi kuzuia watoto wao kuangalia tamthilia zenye maudhui ya kimapenzi.

Amesema tamthilia nyingi zimekuwa zikisababisha mmomonyoko wa maadili kwa watoto.

Alitoa kauli hiyo juzi kwenye maadhimisho ya wiki ya watoto kanisani hapo.

Maadhimisho hayo yaliongozwa na watoto ambao waliongoza ibada pamoja na kuonyesha vipaji mbalimbali, ikiwamo kukariri mistari katika Biblia, kuimba na kufanya maigizo yenye ujumbe wa neno la Mungu.

Alisema katika ulimwengu wa kidijitali wazazi wanapaswa kuwa makini na malezi ya watoto wao, pamoja na kuwazuia kuangalia tamthilia zenye maudhui ya kimapenzi, ambazo kwa sasa ndiyo zimekuwa moja ya chanzo kikubwa cha mmomonyoko wa maadili kwa watoto na kuiga maigizo hayo na kufanya uhalisia.

"Mimi nyumbani kwangu nilipiga marufuku kuangalia tamthilia maana maudhui yake ni mapenzi tu, watoto wakiangalia maigizo hayo wanakwenda kufanya uhalisia, ndiyo chanzo cha mimba za utotoni, usagaji, ushoga na kuvuta dawa za kulevya," alisema Askofu Mabushi.

Aidha, aliwataka wazazi kuwa makini na tamthilia hizo ambazo kwa sasa ndiyo zimeteka akili za watu wengi na kuanza kuishi maisha ya kwenye maigizo, kusahau malezi bora ya watoto wao hali ambayo ni hatari nchi kuja kupoteza taifa la kesho.

Naye Mtoto Vanesa Ephata akisoma hotuba kwa niaba ya wenzake, aliwaomba wazazi wazingatie malezi bora ya watoto wao na kuacha kuwa bize na mitandao ya kijamii, kusababisha mmomonyoko wa maadili kwa watoto kutokana na kukosa usimamizi wa maisha yao.

Aliwaomba pia wazazi wapendane na kuacha tabia ya kugombana mbele ya watoto, pamoja na kutoleana lugha chafu huku wao wakisikiliza kitendo ambacho kimekuwa kikiwaathiri watoto kisaikolojia na kuacha kuwafanyia watoto vitendo vya ukatili.



Ukurasa 14

Kulinda hifadhi kwa mtutu kunavyoweza kumalizwa



Ukurasa 13

Kelele mafuta kupikia, TARI inapozijibu kwa kuleta alizeti mpya

Nipashe

# TESA

Jumanne Juni 27, 2023

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

Uhaba, ukosefu vitabu ulivyokoma shuleni kupitia maktaba mtandao

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

NAO NI UNYANYASAJI

# Usichukulie poa kutumia majina ya vitu, wanyama kukejeli watoto huwaathiri


KUNA mambo yanafanyika kwa mazoea kwenye familia na ndani ya jamii kuanzia na kuwapiga watoto kwa vitu kama ufagio au upawa na kuwatukana kwa majina ya wanyama, yote ikichukuliwa kuwa ni jambo la kawaida.

Kwa mfano, wazazi na walezi wanawapachika majina watoto mfano wee 'domo' sababu ana mdomo mkubwa au 'chauvivu' akidaiwa hawezi kufanyakazi, yote haya watetezi wa haki za watoto wanasema ni unyanyasaji na ukatili.

Unapozungumzia aina ya ukatili wa kijinsia kwa watoto siyo wanafunzi, wazazi au walezi wote wanaofahamu aina za unyanyasaji huo kumbe hata kumwita mtoto majina ya wanyama kama mbuzi au ng'ombe ni ukatili pia.

Hivyo, unyanyasaji unahusisha mengi yakiwamo yanayofanyika majumbani kama kuwapiga watoto na mchi, jalo la kuchotea mkaa, kucharazwa na mkanda, kuchomwa na pasi ya moto, ukeketaji, ulawiti na ubakaji ndiyo matukio ya ukatili wa kijinsia.

Ili kuifahamisha na kuiamsha jamii kuhusu matendo ya ukatili kwa watoto yasiyopewa uzito, hivi karibuni mashirika ya kiraia ya Women in Social Entrepreneurship (WISE) pamoja na Transforming Life, wanawafundisha wanafunzi ya Shule ya Msingi Keko-Magurumbasi jijini Dar es Salaam, aina za ukatili wa kijinsia.



Adhabu kwa watoto zilizopitiliza ni ukatili na unyanyasaji. **PICHA: MTANDAO**

Aidha, wanafahamishwa sehemu za kutoa taarifa wanapofanyiwa ukatili iwe nyumbani, mitaani na shuleni anasema Wakili katika Transforming Life, Theresia Kinabo.

Anaeleza kuwa ni kazi iliyofanyika wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika inayofanyika Juni 16 kila mwaka, kwa kushirikiana na Holt Children's Service Incorporation kutoka Korea Kusini.

Mbali na hilo, wanafunzi wanafundishwa maana ya mtoto, haki, wajibu wao ulinzi wa watoto, anayelinda watoto, maana ya ukatili, aina zake mfano wa kimwili, kisaikolojia, ngono, kupigwa, mimba za utotoni yote kwa kwa mujibu wa sheria ya mtoto ya mwaka 2009.

Aidha, Theresia anasema wakati wa mafunzo, pia wanafunzi wanataka kufahamu maana ya mila na desturi potofu, mfano ukeketaji na walifundishwa na kuelezwa kuwa mtoto akiolewa chini ya miaka 18 haki ya kusoma inakiukwa, hawezi kujua majukumu yake wala ya familia, hivyo ni ukatili pia.

"Kwa sababu mmepata elimu hii, mkiona mzazi au mlezi anafanya matukio ya ukatili wa kijinsia au kuvunja haki zenu toa taarifa kwenye serikali ya mtaa, dawati la jinsia na watoto la polisi, walimu shuleni, mzazi au mlezi ambaye anaweza kukusaidia kapata haki yako." Anasema Theresia.

Akizungumzia ukatili wa kisaikolojia, Theresa anawaasa wazazi na walezi wasiwaite watoto au yeyote mbwa au mbuzi kwa sababu wanawaharibu kisaikolojia, wanapowaza kuwa wanafanana na mbwa au mbuzi, hatawakiwa darasani wanaweza kufeli masomo kutokana na kuitwa majina akihimiza kuita watoto maneno mazuri yenye kuwajenga siyo kuwaathiri kisaikolojia.

### NI ULINZI

Mkurugenzi Mtendaji wa WIS, Dk. Astronaut Bagile, anasema watoto wakielewa haki zao na kujua maana ya ukatili wa kijinsia wanaweza kuchukua hatua na ni sehemu ya ulinzi. "Tumeamua kutoa mafunzo haya kwa sababu kwenye jamii kuna matukio mengi ya ukatili wa kijinsia na ukiwaongezea uelewa watoto wanaweza kuchukua hatua." Anasema.

Astronaut anawaomba wanafunzi kwenda kufundisha rafiki zao nyumbani na wakubwa pia yale waliyofundishwa shuleni kwa ustawi wao na wa taifa.

Zulfa Frank mwanafunzi wa darasa la sita Keko- Magurumbasi anasema waliyojifunza yamewaelimisha kuwa ni lazima watoto wapatiwe haki wanazostahili, lakini wawaheshimu wazazi au walezi, walimu, wafanye kazi kwa kujituma, wawe wakweli," anasema.

Anaeleza kuwa kilichomvutia katika masomo haya ni mbinu na sehemu za kutoa taarifa wanapofanyiwa vitendo hatarishi, kama vile kunyanyaswa kingono, ukeketaji, kupigwa, kuumizwa, kutishwa pale anapofanyiwa kitendo hatarishi kama kusema nitakuua au kuua wazazi au walezi wake.

Mwalimu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA Keko Magurumbasi, Daha Berther, anasema wanafunzi 650 walifundishwa uimarishaji ulinzi na fursa sawa kwa watoto na maendeleo endelevu 2030.

"Elimu hii ni bora kwa sababu wamepata watu kutoka nje ya shule, mtoto ana shika zaidi anachofundishwa na wageni kuliko sisi wa kila siku shuleni ingawa masomo mengine yapo kwenye somo la uraia," anasema.

Watoto wameelewa kuhusu unyanyasaji kwenye jamii, wanaripoti kesi, mtoto anapigwa na mwiko, wengine wameunguzwa na moto wamejua kuwa huo pia ni ukatili wa kijinsia na wanauripoti.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI

# Uhaba, ukosefu vitabu ulivyokoma shuleni kupitia maktaba mtandao




Watoto wakifurahia vitabu mbalimbali katika maktaba. **PICHA: ROOM TO READ**

MBINU mbalimbali zinatumika kuwawekea watoto mazingira wezeshi kusoma na kufundishiwa ili wapende shule na kuondokana na utoro unaosababisha ongezeko la 'mambumbumbu'.

Vitabu vya hadithi ni mbinu inayowavutia watoto kutaka kujua kusoma kwa haraka ili kujua kilichoandikwa pia kwenda shule kupata vitabu zaidi ili kujisomea.

Ili kufanikisha kupata vitabu vingi vya hadithi ambavyo vitawawezesha watoto kubadilisha mitizamo na kujisomea na kujifunza mambo mbalimbali kunahitaji maktaba shuleni.

Francis Likwe ni Mratibu wa Maktaba Mtandao kutoka shirika la kiraia la Room to Read, anayesema ni moja ya asasi ambayo yamekuwa yanaendesha miradi mbalimbali shuleni ikiwamo ya maktaba inayohamasisha watoto kupenda shule na kujua kusoma na kuandika kwa haraka.

Anasema katika miradi ya maktaba shirika hilo limefikisha maktaba 337 kwenye baadhi ya mikoa ikiwamo Pwani ambayo kwenye shule zenye maktaba 337 matokeo chanya yameonekana.

Anasema hata hivyo, mbali ya kuwa na maktaba za kawaida kwenye baadhi ya shule shirika hilo lilianzisha mradi mwingine wa maktaba mtandao wakiwa na lengo la kukuza stadi za usomaji na kukuza tabia ya usomaji wa vitabu vya hadithi.

> Hizi shule 20 ni za majaribio mbali ya kupewa vitendea kazi hivyo pia kuna fedha kwa ajili ya bando tunawatumia kila mwezi ili kutekeleza vizuri majukumu yao ya kuwafundisha wanafunzi.

Likwe anaeleza kuwa mradi huo wa majaribio umefanyika katika shule 20 mkoa wa Tanga ambazo ziliwezeshwa vishikwambi pamoja na projekta kwa ajili ya kufundishia.

Anaeleza kuwa mradi huo unatekelezwa katika Wilaya za Handeni, Korogwe, Muheza na Tanga Mjini na kwamba kila shule imepata kishikwambi pamoja na projekta.

"Hizi shule 20 ni za majaribio mbali ya kupewa vitendea kazi hivyo pia kuna fedha kwa ajili ya bando tunawatumia kila mwezi ili kutekeleza vizuri majukumu yao ya kuwafundisha wanafunzi," anasema Likwe.

Mratibu huyo anaeleza kwamba maktaba mtandao inamwezesha mtoto sehemu yoyote kujisomea kupitia simu kubwa na kishikwambi vitabu mbalimbali vya hadithi kwa lugha tofauti.

Aidha, anasema kupitia njia hiyo pia watoto watasoma vitabu kupitia video ambazo zinasimulia hadithi zinazomshawishi mtoto kuwa na hamu ya kujua kusoma ili aweze kujifunza vitu vingi kupitia hadithi.

Anasema kupitia mradi huo watafanya tathmini ya nini kifanyike zaidi ili kuwawezesha watoto wengi kupenda kusoma hatua ambayo itaondoa utoro na kuwainua kwenye ufaulu wa mitihani ya kujipima na kitaifa.

Kwa mujibu wa mratibu maktaba za awali zilikuwa zikiwanufaisha wanafunzi walio kwenye mradi pekee lakini za mtandao ni rahisi kwa kuwa watoto wengi watanufaika popote walipo.

Anasema elimu kuhusu maktaba mtandaoni wamekuwa wakitoa kwenye maeneo ambayo wanatekeleza miradi yao mingine na hivyo wazazi na wanafunzi kunufaika na kutumia simu walizonazo kujisomea vitabu mbalimbali vya hadithi.

Mkurugenzi wa Uendeshaji na Utekelezaji wa Miradi Room to Read, Magdalena George, akizungumza katika Siku ya Mtoto wa Afrika iliyoadhimishwa kwa kukutana na watoto wa shule ya msingi, anasema wanafanya kazi na serikali katika kuhakikisha wanakuza ujuzi wa kusoma na kuandika na kujenga tabia ya usomaji.

Shirika hilo pia limekuwa likisaidia wasichana kumaliza sekondari wakiwa na stadi muhimu zitakazo wawezesha kufanya kwa maamuzi ya msingi katika maisha yao ili wafanikiwe shuleni na zaidi.

Magdalena anasema katika miradi miwili inayotekeleza na shirika hilo la usomaji na maktaba na mradi wa elimu kwa msichana imewalenga watoto kuhakikisha kuwa wanalinda haki za mtoto wa Afrika.

"Tuweke sera ya ulinzi wa mtoto ili ilindwe dhidi ya unyanyasaji, uonevu, kupuuzwa, ukatili wa kimwili kingono na kudhuru mwili, sera hii imethibitisha kujitoa kikamilifu kwa Room to Read katika elimu na ustawi wa watoto," anasema Magdalena.

Aidha anasema inaamini dunia ya kidijitali inaweza kuwa na matokeo chanya kwa watoto endapo utatumika vizuri na kwamba wanathamini maendeleo ya TEHAMA jambo ambalo limewasababisha kuanzisha maktaba mtandao iliyosheheni vitabu mbalimbali vikiwamo vya Kiswahili.

Mkurugenzi huyo anabainisha kwamba maktaba mtandao inatatua kikwazo cha ukosefu wa vitabu vizuri vya hadithi lakini kumlinda mtoto kwa kigezo cha matumizi ya muda.

"Maktaba mtandao pia inaweza kutumiwa na walimu, wazazi na wadau wa elimu kujisomea na kupata rasilimali mbalimbali za usomaji na pia ndiyo sehemu pekee ambayo mtoto anaweza kupata fursa ya kuendeleza stadi za kusoma alizojifunza darasani na kujenga tabia ya usomaji."

"Shirika letu limeshuhudia mabadiliko chanya kadhaa ikiwamo watoto kupenda kujisomea shuleni na nyumbani, kuwahi shule ili kwenda kuazima vitabu maktaba kupunguza kelele na utoro na kuwawezesha kufanya vizuri kwenye masomo yao," anabainisha Magdalena.

Bernad Lulanda ni mwalimu wa Shule ya Msingi Muheza wilayani Muheza anaeleza kuwa maktaba mtandao imekuwa mkombozi kwa watoto waliokuwa hawapendi kusoma.

"Walikuwa wanataka kwenda maktaba kuangalia video na hii ikawahamasisha wale ambao walikuwa hawajui kusoma sasa kujifunza kwa bidi kusoma na kuandika, lakini pia imepunguza utoro," anaeleza.

Lulanda anasema hadi sasa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la tatu wengi wao wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu na hilo limechangiwa na uwepo wa maktaba mtandao.

Aidha, amefikisha maombi yake Room to Read kwa ajili ya kuongeza vitabu vya hadithi vyenye mvuto ili wanafunzi wasome zaidi na kujifunza kupitia maktaba mtandao.

TEKNOLOJIA

NA MAULID MMBAGA

## KELELE MAFUTA KUPIKIA

# TARI inapozijibu kwa kuleta alizeti mpya

• Hutoa madumu 16 kwa ekari badala ya tatu

MABADILIKO ya hali ya hewa yenye athari kuanzia kuongeza joto na ubaridi, ukame, mafuriko, vimbunga na tufani vyote vikiathiri kilimo na kusababisha njaa na upungufu wa chakula hayajaiacha salama Tanzania.

Athari mbaya kwa hali ya hewa kwenye kilimo zinalifikirisha taifa na vyombo vinavyokisimamia mathalani, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) ambayo imejibu kwa kubuni teknolojia za kupata mbegu zenye mavuno zaidi, zinazovumilia ukame, wadudu waharibifu pia kukomaa haraka.

Kituo cha TARI Ilonga kilichoko Morogoro, ni miongoni mwa taasisi za kilimo kinachoratibu utafiti wa alizeti na mazao jamii ya mikunde chini ya mradi wa Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT) unaohamasisha matumizi ya mbegu bora, kupima udongo na kuwabadilisha wakulima ili kuondokana na kilimo cha mazoea.

Mkurugenzi wa TARI Ilonga, Dk. Emmanuel Chilagane, anasema uzalishaji wa mbegu za alizeti uko chini na uwepo wadau kama AMDT unaongeza upatikanaji mbegu bora, akiungwa mkono na mtafiti Beatrice Inko, anayesema wanafanya jaribio la vinasaba vya alizeti vilivyokusanywa kutoka maeneo mbalimbali duniani kugundua jamii bora itafanikisha kupata mbegu bora.




Meneja Uzalishaji wa Kampuni ya Highland Seed Growers wanufaika AMDT, Iddi Omari, akionyesha namna mbegu bora ya alizeti inavyozaa kwa ukubwa. **PICHA: MAULID MMBAGAA**

### KURUTUBISHA UDONGO

Ofisa Kilimo Idara ya alizeti TARI Ilonga, Witnesspeacequen Ikundi, anasema wanafanya tafiti za kurutubisha au kuongeza rutuba kwenye udongo baada ya kubaini wakulima wengi wanalima zao moja misimu yote.

Anabainisha kuwa kulima zao moja kunakofanywa na wakulima wengi kunasababisha udongo kupoteza rutuba licha ya kwamba wengi hawana uwezo wa kumudu gharama za mbolea za viwandani.

"Ili kurudisha rutuba tunafanya utafiti kujua marejeo yanaongeza kiasi gani cha rutuba kwenye udongo, na kwa sasa mazao ya jamii ya mikunde ni chanzo cha kurejesha rutuba shambani," anasema Ikundi.

Aidha, wanachukua sampuli za udongo na kuzipima ili kujua naitrojen na karboni ziko kwa kiasi gani kwenye ardhi, ili kuwaelimisha wakulima kufanya kilimo mzunguko kwa kubadilisha mazao kila msimu.

"Niwashauri kutumia kilimo mzunguko mfano akilima alizeti, akivuna apande jamii ya mikunde kabla ya msimu mwingine, asilime zao moja muda wote kwa mfululizo ili kurudisha rutuba ya udongo," anasisitiza Ikundi.

Msimamizi wa mradi huo wa alizeti Frank Reuben, anasema juhudi zinafanywa ili wakulima wenye kuhitaji wapate mbegu bora licha ya mahitaji kuwa makubwa akiongeza kuwa wanazalisha kilo 100,000 za mbegu inayopandwa kwenye ekari 50,000 msimu ujao.

"Ili kuzalisha mbegu za kutosha AMDT wanashauri ni muhimu kuwapo ubia kati ya serikali na sekta binafsi, sisi TARI hilo tumelitekeleza, fedha tunazozipata tunazitumia na kampuni za mbegu tunazoshirikiana nazo na tunazijengea uwezo wa kuzalisha mbegu bora, kwa kuwapa mafunzo na kufuatilia ili wanachokizalisha kikidhi vigezo," anasema Reuben.

Ofisa ugani wa kampuni ya Ikuo iliyoko Sumbawanga mkoani Rukwa, Amos Songolo, anasema wanatoa elimu inayowawezesha wakulima kujua namna ya kuandaa shamba, kupanda na kutunza mimea na shamba ili kufikia kilimo chenye tija.

"Kingine mradi unachokifanya ni kuwasaidia wakulima kupima sampuli za udongo ili wajue mbolea inayowafaa na kwa kiasi gani kulingana na ukubwa wa shamba," anasema Songolo.

Anasema mafunzo wanayoyatoa wamewafikia wakulima zaidi ya 5,000 wanaohitaji mbegu bora.

### UWEZESHWAJI

Mtendaji Mkuu wa AMDT, Charles Ogutu, anasema imewekeza bilioni nne kuendeleza kilimo cha alizeti na mazao ya mikunde katika mikoa 11 kwa kushirikiana na TARI, ikieleza kuwa fedha hizo ambazo ni sehemu ya ruzuku ya Shilingi bilioni tano iliyotolewa na nchi za Denmark na Sweden zinalenga kuwawezesha wakulima zaidi ya 100,000 katika mikoa ya Manyara, Singida, Dodoma, Lindi, Mtwara, Songwe, Ruvuma, Njombe na Rukwa.

Anataja upatikanaji mbegu bora, kuboresha ugani, usimamizi wa mavuno na uchakataji wa alizeti ili kuongeza thamani, kuwa ni maeneo yanayokuwa na uwekezaji huo.

"Miradi yote inazingatia masuala mtambuka ya ushiriki wa wanawake na vijana pamoja na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa ili kujenga ustahimilivu kwa wakulima," anasema Ogutu.

Mkulima wa alizeti Braunes Chengula, mkazi wa Wilaya ya Wanging'ombe, mkoani Njombe, anaeleza kuwa mbegu hizo zilizoboreshwa zinatoa mavuno mengi na kwa ekari uvunaji umeongezeka kutoka madebe manne hadi 20.

> Gharama wanazozikimbia ni hatua ya kuandaa shamba, kununua mbegu za kisasa ambazo utofauti wake na zingine zinazaa na zinavumilia mabadiliko ya hali ya hewa.

Anasema ni mwaka wa pili sasa tangu ameanze kutumia mbegu bora ya alizeti na maharage, na kushukuru AMDT kuwawezesha wakulima wadogo wa vijijini kupata mbegu bora ambazo ni mkombozi wa wakulima.

"Tangu nilipoanza na sasa najiona nimepiga hatua, nilikuwa nalima ekari nne lakini sasa zinafika 10 kwasababu tija ya kilimo cha kisasa na kutumia mbegu bora ninaiona," anasema Braunes mama wa watoto wane.

"Awali wakati tunatumia mbegu za kawaida ukipata madebe matatu unaona umevuna, lakini kwa sasa baada ya kuanza kutumia mbegu bora nikipata maharage madebe 10 kwa ekari najiona nimekosa sana, na waasa wengine wajiunge na kilimo hiki kina manufaa makubwa."

Zuhura Mpinga, mkazi wa Kijiji cha Mayale Njombe, anasema unapotumia mbegu bora za alizeti zinazoshauriwa na wataalamu hata kama mvua itapungua huwezi kukosa mavuno kwenye ekari moja mbegu mpya hutoa wastani wa debe 80, ambazo ukizikamua unapata mafuta madumu 16 ya lita 20.

"Kwa sasa nimepiga hatua kubwa kwa sababu ninafanya kilimo mkataba na vijiji karibu vitano, ikiwemo kijiji cha Ufwala ambacho kina wakulima takribani 200, Ruduga A, B hadi C kuna wasiopungua 150, ambao nimekuwa nikiwauzia mbegu halafu malipo nayapata baada ya mavuno," anasema Zuhura.

Osward Mtindiya, ambaye ni mkulima wa maharage na mnufaika wa mradi wa kilimo himilivu mkoani Rukwa, anasema baadhi ya wakulima mkoani humo wanakwepa gharama zinazohitajika kwenye kilimo na kwamba hiyo ni moja ya kigezo kinachosababisha waendelee kubaki na umaskini, akiwasisitiza kufuata elimu ya kilimo bora.

"Gharama wanazozikimbia ni hatua ya kuandaa shamba, kununua mbegu za kisasa ambazo utofauti wake na zingine zinazaa na zinavumilia mabadiliko ya hali ya hewa," anasema Mtindiya.

Hata hivyo, mafanikio hayo ya wakulima ni moja ya maleo makubwa ya serikali na AMDT kama anavyo bainisha Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Jenifa Omolo.

Anasema lengo la serikali kuongeza bajeti katika sekta ya kilimo ni kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora, kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na kutoa elimu kwa wakulima.

ELIMU
NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Kulinda hifadhi kwa mtutu kunavyoweza kumalizwa

• Wananchi watakuwa wanufaika namba moja kila programu

SERA ya Misitu ya 1998, inaeleza kuwa Wakala wa Misitu, anaweza kutumia kifungu kinachohusu kukasimu usimamizi au uendelezaji wa mashamba ya miti na misitu ya asili ya uzalishaji kwa makubaliano maalumu kwa faida ya wote.

Ikifanyika hivyo, taifa litanufaika zaidi maana sekta binafsi wanaweza kufanya kazi kwa umakini zaidi wakifahamu watengeneze bidhaa gani kulingana na mahitaji ya soko la ndani na la duniani.

Sekta hii haitatumia magogo kutengeneza karatasi wakati malighafi ipo na inaoza kwenye shamba la miti. Hatuna sababu ya kuagiza karatasi nje kwa gharama ya Dola za Marekani zaidi ya milioni 100 kwa mwaka wakati uwezo wa kuzalisha karatasi upo.

Vilevile, kutakuwapo ushindani wa kibiashara na kulinufaisha taifa, kinachotakiwa ni sera na mifumo ya kisheria wezeshi na rafiki kwa sekta binafsi kuchangamkia fursa zilizopo katika misitu na nyuki.

Kiini cha kuanzisha wakala ilikuwa kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shughuli za misitu na nyuki, kuwapo mabadiliko chanya mfano kuboresha huduma za misitu kiikolojia na mazingira kuhakikisha mapato yanaongezeka bila kuharibu ikolojia ya misitu kwakujikita katika misingi ya kitaaluma na endelevu.

Kila ninapopita sehemu mbalimbali nasikia kilio cha wadau wengi wakisema 'misitu imeharibika sana' kiwango cha kukatishana tamaa'. Mapema mwaka huu nilitembelea Morogoro, nilikutana na mtu aliyenifahamu, baada ya kusalimiana akanipongeza kwa kazi nzuri niliyoifanya.

Nikamwambia lakini sasa ni zaidi ya miaka 10 iliyopita tangu nitoke serikalini, akasema 'pamoja na hayo, bado baadhi yetu tuna kumbukumbu zako maana ulikuwa mstari wa mbele kuilinda na kuitetea misitu' huku akitoa mfano wa misitu kwenye Milima ya Uluguru.

Wakati tunaendelea na mazungumzo akajitokeza mzee mwenye umri mkubwa zaidi kwake, wakasalimiana na akamfahamisha jina langu na yule baba akasema." Eeh kweli ni mtu muhimu sana kwa mazingira'. Ndipo akaongeza kuwa iwapo misitu ingekuwa na macho na sauti, na umefika kwenye hii ya Milima ya Uluguru, baada ya kumuona ingepiga kelele na kulia machozi ikimwambia mbona umetutelekeza kiasi hicho maana hatuna amani, mashoka na misimeno vimezidi, tunaumia".

Sikujibu kitu nilibaki nashangazwa na kauli za hao wazee. Nikajiuliza picha kama hii maana yake nini? Hata hivyo wahenga walisema, "yaliyopita si ndwele tugange yajayo. Vilevile, nimekuwa nikisikia baadhi ya watu wakisema "yajayo yanafurahisha".



Udhibiti wa majangili kwa silaha ukifanywa na walinzi wa hifadhi. **PICHA: MTANDAO**

> Wapo wasioamini lakini ni 'roho za ubinafsi na kujipenda zaidi kuliko kuwapenda walio wengi mijini na vijijini.

Natamani kauli hiyo itimie kwenye usimamizi, uendelezaji na utumiaji wa rasilimali misitu na nyuki hadi kuwepo matokea yanayowafurahisha Watanzania.

Kama tukiamua kufanya kweli hakuna kinachoshindikana katika dunia hii tunayoishi na kwa muda mfupi hayati John Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano, amewafungua macho wengi kwa kudhihirisha kuwa tunaweza kufanya makubwa kwa nchi hii ndani ya muda mfupi na yote yanawezekana kwake aaminiye.

Wapo wasioamini lakini ni 'roho za ubinafsi na kujipenda zaidi kuliko kuwapenda walio wengi mijini na vijijini.

Kiroho, tunatakiwa kuwapenda majirani zetu kama tunavyozipenda nafsi zetu unachotakiwa ukipate na jirani yako akipate. Nimewahi kumuona kupitia mitandao ya kijamii, Prof. Patrick Loch Otieno Lumumba wa Kenya akisema alitamani katika Bara la Afrika kufanyike kitu kama "Magufulification".

Kama nilimwelewa vizuri nia yake ilikuwa kuiona Afrika inajiletea maendeleo endelevu kwa muda mfupi ujao kuliko kukaa miaka mingi ya kutegemea misaada ya wahisani huku kukibaki bila kusonga mbele ipasavyo.

Katika sekta ya misitu na nyuki, bado iko nafasi ya kufanya vizuri Tanzania ikidhamiria ipasavyo itafanikiwa. Kinachotakiwa ni kubadili mitazamo, fikra, na kuweka mbele masilahi ya taifa zima.

Siasa na sera zetu pamoja na sheria, kanuni na utaratibu vizingatie kuwa serikali haiwezi, peke yake, kuisimamia na kutunza rasilimali ikiwamo misitu na nyuki bila kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo wananchi wanaoishi katika vijiji na vitongoji karibu na maeneo ya misitu hasa yaliyohifadhiwa. Kadhalika, misingi ya taaluma ya misitu na nyuki izingatiwe ipasavyo. Siasa na sera pamoja na sheria, visikinzane na kanuni za kitaalamu (professional principles and ethics).

**MAPENDEKEZO**

Sekta binafsi ipewe nafasi katika kuotesha, kutunza, kusimamia mashamba ya miti hadi kutengeneza bidhaa. Kupanda na kuendeleza mashamba ya miti kibiashara. Hivyo, namaanisha kuiwezesha sekta-binafsi kutumia ardhi ya umma kwa kuiendeleza kibiashara kupitia upandaji miti na kuzalisha bidhaa kwa makubaliano maalum na serikali.

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, wabaki na usimamizi wa kisera na kisheria na kuhakikisha taifa linanufaika kupitia mapato kulingana na makubaliano kisheria.

Aidha, iwapo hilo litatekelezwa ipasavyo, wataalamu wa misitu na nyuki waliopo wawekeze nguvu zao kuilinda na kuisimamia misitu ya asili na nyuki pamoja na viumbe wengine adimu kwa faida ya wote.

Halikadhalika iandaliwe programu maalum itakayowawezesha wadau na wananchi waishio vijijini na vitongojini kuwapatia elimu ya mara kwa mara na kuweka utaratibu wa kuwahusisha katika shughuli za kulinda misitu na nyuki kwa faida ya wote.

Uzoefu unaonyesha kuwa wadau, wananchi wakielewa umuhimu wa misitu na faida zake kwa maisha yao, hakika watafanya kweli. Lakini wakiona hawahusishwi watafanya wanayoyajua wenyewe hivyo rasilimali hiyo inakuwa kama 'mashamba ya bibi'.

Pamoja na hayo, suala la wataalam wa misitu kubadilike lazima liwepo tulisomee taaluma za misitu na nyuki ambazo kiuhalisia rasilimali zake ziko vijijini.

Wapo wachache ambao watatakiwa kuwa mijini lakini walio wengi twende tufanye kazi katika maeneo ya misitu tunayotakiwa kuisimamia na kuiendeleza. Hii inamaanisha kuhamia na kukaa sehemu misitu iliko (in-situ) na kuhakikisha misitu inalindwa ipasavyo.

Huko tutengeneze miundombinu ikiwamo ofisi, nyumba za watumishi na iwapo huduma za afya ni mbali kujengwe zahanati na barabara ziimarishwe wataalamu wa barabara msitu wapo na wanaweza pia kuimarisha barabara vijijini. Vifaa matingatinga vipatike kwenye kanda siyo kwa kila msitu na kazi ifanyike ipasavyo.





## Taasisi za fedha, dini zaitwa kuwasaidia wenye uhitaji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

TAASISI za kifedha, mashirika ya dini, wadau wa maendeleo na watu binafsi wameombwa kusaidia jamii zisizo na uwezo, zinazoishi katika kambi ya wagonjwa ya Msamaria iliyopo Hombolo Jijini Dodoma ambao wanakabiliana na ukosefu wa dawa, chakula, mavazi, maji na umeme.

Ombi hilo limetolewa na Meneja wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Mohamed Masoud alipokuwa akikabidhi sehemu ya dawa za kusafisha na kutibu vidonda kwa wagonjwa wa ukoma wa kituo cha Msamaria kilichopo Hombolo Jiji la Dodoma.

Alisema wagonjwa hao wa kambi hiyo wanakabiliwa na kero nyingi, hivyo wanatakiwa kuangaliwa kwa ukaribu kwa kuwasaidia misaada mbalimbali inayohitajika kama vile matibabu, chakula mavazi, elimu na mikopo nafuu watakayoweze kumudu kurejesha.

Meneja huyo aliziomba taasisi za kifedha, mashirika mbalimbali yakiwemo ya kidini na watu binafsi kuelekeza misaada yao kwa jamii hizo ili waweze kuondokana na hali duni walizonazo.

"Nafahamu kituo cha Msamaria cha Hombolo kilichopo Jiji la Dodoma kuna wenye uhitaji wengi hivyo ni muhimu taasisi, mashirika na wadau wa maendeleo kuelekeza misaada mbalimbali ili waweze kutatua kero walizonazo ndani ya familia zinazoishi kwenye kambi hiyo," alisema.

Naye Charles Chiboko na Rozi Ufinyu ambao ni wagonjwa wa ukoma wa kambi hiyo ya Msamaria Hombolo, wakizungumza baada ya kupokea msaada huo walisema bado wanakabiliana na kero nyingi zinazowafanya kuonekana kuwa jamii imewatenga.

"Familia zinazoishi hapa zinakabiliwa na matatizo mengi hivyo tunaziomba taasisi za fedha, mashirika ya dini na wadau mbalimbali wa maendeleo kutuangalia kwa jicho la pili ili tuondokane na shida zinazotukabili zikiwamo hili la kukosa dawa, chakula mavazi na fedha za kujikimu kimaisha," alisema.

Aidha, alisema familia zinazoishi kwenye kambi hiyo zinaonekana zimetengwa na kusahaulika kutokana na kukosa mahitaji muhimu kama ilivyo kwa wanadamu wengine ambao wanapata huduma zikiwemo dawa, elimu, mavazi, fedha za kujikimu na chakula.

Naye Mratibu wa huduma ya matunzo katika kituo hicho cha Msamaria cha Hombolo Philimon Ulanga alisema dawa zilizotolewa ni kwa ajili ya kusafisha na kutibu vidonda hata hivyo bado kuna uhitaji mkubwa.

# Polisi yaanza ukaguzi vyuo vya udereva kuzuia ajali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JESHI la Polisi limeanza ukaguzi wa vyuo vya mafunzo ya udereva ili kukabiliana na ongezeko la ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara katika maeneo mengi ya nchi, huku likisisitiza kuwa vitakavyobainika kukosa sifa vitafungiwa.

Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi na Mkuu wa Dawati la Elimu ya Usalama Barabarani, Michael Deleli, aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na wamiliki wa vyuo vya mafunzo ya udereva mkoani Dodoma.

Alisema ukaguzi wa vyuo hivyo unalenga kubaini kama vinakidhi vigezo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Camillius Wambura.

Aidha, aliwataka wamiliki wa vyuo vya mafunzo ya udereva nchini kutoa mafunzo ambayo yanaendana na teknolojia ya sasa sambamba na kusimamia maadili ya kazi hiyo.

Alisema hivi sasa ajali nyingi zinatokana na makosa ya kibinadamu kutokana na madereva wengi kuendesha vyombo vya moto bila kuzingatia sheria za usalama barabarani na wakati mwingine kutotambua wajibu.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa kwa kipindi cha mwaka 2022 madereva wengi waliofanyiwa uhakiki wa leseni hawakupitia katika vyuo vya udereva na hawakuwa na leseni.

"Asilimia 75 ya ajali inatokana na makosa ya kibinadamu, asilimia 15 vyombo vyenyewe na asilimia tano ni miundombinu, inaonesha wazi kuwa makosa ya kibinadamu yanaongoza kwa kusababisha ajali hiyo inatokana na kuwa na madereva wasiokuwa na nidhani ya kazi na wakati mwingine kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya chombo anachokiendesha," alisema.

Kutokana na hali hiyo aliwashauri wamiliki wa vyuo vya udereva kuhakikisha wanawatafuta walimu wenye elimu ya magari ili mwanafunzi anapokuwa akijifunza aweze kujifunza mifumo mbalimbali ya magari, kumrahisishia kutambua tatizo haraka pale linapotokea akiwa barabarani.

Kadhalika, alisema elimu ya usalama barabarani bado ni kikwazo kwa Watanzania hivyo ni wajibu wa kila mtu mwenye uelewa juu ya usalama barabarani kutoa elimu kwa jamii inayomzunguka ili kukabiliana na hali hiyo.

Mwenyekiti wa Wamiliki wa Vyuo vya Udereva Mkoa wa Dodoma, Robert Mwinje, alisema watazingatia ushauri na maelekezo ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya kuhakikisha wanaendesha mafuzo kwa kutumia walimu wanaokidhi mahitaji ya soko la sasa.

Hata hivyo, alisema pamoja na kuwapo kwa mafunzo hayo bado wanakabiliwa na ukosefu wa maeneo makubwa ya kufundishia huku akiahidi wamiliki wa vyuo vya udereva kushirikiana na serikali ili kupunguza ajali za barabarani ambazo ni tishio kwa nguvu kazi ya taifa.



Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Camillus Wambura (wa pili kushoto), akiwa na ujumbe wa Bank of Africa Tanzania ukiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Adam Mihayo (wa pili kulia), alipomtembelea ofisini kwake jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Wengine ni Derick Lugemala, Mkuu wa Kitengo cha Fedha (kushoto) na Nandi Mwiyombella ambaye ni Mkuu wa Masoko na Mawasiliano. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utitiri wa leseni wawakera wamiliki hoteli

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHEMBA ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Singida imezilalamikia halmashauri za mkoa huo kwa kutoza leseni nyingi wawekezaji wenye hoteli wakisema inapunguza uwezo wa kushindana kibiashara na hivyo kufukuza baadhi ya wateja wa hadhi ya kima taifa.

Mwenyekiti wa TCCIA Mkoa wa Singida, Kitila Katala, alimweleza hayo Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba kuhusu changamoto hiyo wakati wa kikao cha Baraza la Biashara la Mkoa.

Katala alisema wawekezaji wa hoteli mkoani Singida wanapewa leseni nyingi pasipo sababu na kusababisha mzigo mkubwa ambao unawafanya washindwe kushindana kibiashara na mikoa mingine.

"Hoteli za hapa Singida zina leseni ya ukumbi, baa, mgahawa, duka na nyumba ya kulala wageni, hatuna leseni ya hoteli, huu mlolongo ni mzigo mkubwa na unapunguza uwezo wa kushindania tenda na sehemu nyingine kwani tunaonekana hatuna hoteli," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Mwenyekiti huyo wa TCCIA aliziomba halmashauri kufanya marekebisho ya utozaji leseni kwa wawekezaji wa hoteli, wawe wanatozwa leseni moja badala ya hizo tano wanazotozwa sasa.

Aidha, Katala alisema uingizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi umeathiri bei ya zao la alizeti na mafuta ya alizeti kuwa na ushindani mkubwa na mafuta kutoka nje.

"Tunapendekeza mafuta ya nje yatozwe ushuru kulinda bei kwa mazao ya mkulima na pia bei ya mafuta viwandani, Mkoa wa Singida utaathirika kiuchumi sana kama hali hii itaendelea ya mafuta kutoka nje ya nchi kutotozwa ushuru," alisema.

Kuhusu kukuza uchumi wa Mkoa wa Singida, alisema maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji kwenye halmashauri yafahamike na mamlaka za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Barabara (TANROADS), Wakala wa Barabara Mijiji na Vijijini (TATURA) na maji ili waelekeze miundombinu huko kuvutia wawekezaji.

Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliahidi kuyafanyia kazi mapendekezo hayo.





# CCM Mbeya yaanza ujenzi ofisi za kisasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimeanza mchakato wa kujenga ofisi za kisasa ambazo zinaendana na hadhi ya chama hicho kwa maelezo kuwa ofisi za sasa hazina hadhi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya chama hicho pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema chama hicho kimeunda kamati maalumu ya kuratibu ujenzi wa ofisi hizo ambayo inawahusisha wadau mbalimbali wa chama hicho na kwamba mradi huo ni miongoni mwa kazi ambazo chama hicho kimejiwekea kwenye mipango yake.

Mwaselela alisema kabla ya kuanza ujenzi huo, chama hicho kimeshaanza kuboresha ofisi za chama katika wilaya mbalimbali za mkoa huo ikiwamo Kyela na Rungwe.

"Tunamshukuru Mwenyekiti wetu, Dk. Stephene Mwakajumilo, kwa kuanzisha mchakato wa ujenzi wa ofisi, ameunda kamati maalumu ambayo inaratibu ujenzi wa mradi huu na lengo letu ni kuwa na ofisi ya kisasa," alisema Mwaselela.

Alisema katika Wilaya ya Kyela ofisi tayari imeshaezekwa na kwa sasa kilichobakia ni umaliziaji huku Wilaya ya Rungwe wakiwa wanajiandaa kuezeka.

Katika hatua nyingine Mwaselela alisema chama hicho kimeanzisha utaratibu maalumu wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi ambapo mwenyekiti wa chama hicho anasikiliza kero hizo kila siku ya Jumanne na Alhamisi ya kila wiki.

Hata hivyo Mwaselela alisema chama hicho kimeanza kufuatilia miradi mbalimbali ya chama hicho katika maeneo yote ili kuhakikisha inatumika kwa maendeleo ya chama badala ya kuwanufaisha watu binafsi. Alisema baada ya kamati hiyo kukamilisha kazi watahakikisha wanawachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kuwa wanafuja mali za chama hicho.

Kuhusu uhai wa chama hicho, Mwaselela alisema chama hicho kinakubalika kwa wananchi kutokana na utekelezaji mzuri wa miradi ambayo inawagusa wananchi moja kwa moja.

"Tunaishukuru serikali yetu kwa utekelezaji wa miradi, kuna eneo Chunya wananchi walikuwa wanasafiri kwa Sh. 17,000 kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara lakini kwa sasa wanafika kwa Sh. 7,000 baada ya kujengwa barabara ya lami," alisema Mwaselela.

Alisema chama hicho kimetoa maelekezo kwa viongozi wa serikali katika ngazi zote za mkoa huo kuhakikisha wanasikiliza kero za wananchi na kuzitatua ili wananchi waendelee kuiamini serikali yao.

Alisema yeye kwa nafasi yake amesaidia watendaji wa chama katika ngazi ya wilaya kupata pikipiki ambazo zitawasaidia kuwafikia wananchi na kuwasikiliza ili kuendelea kukiimarisha chama.

Alisema chama hicho kitahakikisha kinawatumikia wananchi vizuri ili waendelee kukiamini na kukifanya kiendelee kubaki madarakani kwa muda mrefu.




Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, Ndele Mwaselela, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Mbeya kuhusu maendeleo ya chama hicho pamoja na utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020/2025 jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Ujenzi barabara ya changarawe wamkosha mbunge

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MBUNGE wa Lupa wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, Masache Kasaka ameridhishwa na ujenzi wa Barabara ya Kiwanja – Ifumbo yenye urefu wa zaidi ya kilomita 10 inayojengwa kwa kiwango cha changarawe akieleza kuwa itasaidia kuboresha mawasiliano.

Mwishoni mwa wiki Kasaka alifanya ziara ya kukagua barabara hiyo kwa lengo la kuangalia utekelezaji wake pamoja na kuzungumza na wananchi wa Kata ya Ifumbo ambao ndio wanufaika wa kwanza wa barabara hiyo.

Alisema barabara hiyo awali ilikuwa na hali mbaya na ilikuwa haiwezi kupitika kwa kutumia gari kutokana na kuwa na makorongo mengi, hali iliyokuwa inawalazimu wananchi wa eneo hilo kutumia gharama kubwa kwenye usafiri.

Alisema usafiri wa uhakika kutumika kwenye eneo hilo ilikuwa ni pikipiki na watembea kwa miguu lakini kwa wenye magari walikuwa wanashindwa kufika.

"Sasa naona imekuwa na hali nzuri na nina uhakika magari ya aina yoyote sasa yanaweza yakafika kwenye eneo hili, kwa hiyo niwaombe wananchi wa Ifumbo muitunze miundombinu hii," alisema Masache.

Aliwapongeza watendaji wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wilayani humo kwa kusimamia vizuri ujenzi wa barabara hiyo na kuifanya kuwa na uwezo wa kupitika mwaka mzima.

Alisema wilaya hiyo ina shida ya barabara, kwamba nyingi kutopitika hususani msimu wa mvua na hivyo akawataka kuendelea kuzifanyia maboresho barabara hizo mara kwa mara ili ziendelee kuwa na hali nzuri.

# Taasisi za fedha zatakiwa kutoa elimu kabla ya utoaji mikopo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI za kifedha mkoani Mbeya zikiwamo benki, zimetakiwa kutoa elimu kwa wananchi kabla ya kuwapatia mikopo ili kuepuka matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza wakati wa urejeshaji wa mikopo hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyasema hayo jijini Mbeya mwishoni mwa wiki wakati wa chakula cha jioni kati ya Benki ya Akiba (ACB) na wateja wake.

Mbali na chakula hicho cha jioni, pia benki hiyo ilitumia muda huo kutambulisha huduma mbalimbali ambazo inazitoa pamoja na kubadilishana mawazo na wateja wa benki hiyo.

"Kumekuwa na tatizo wakati wa ulipaji mikopo kwa baadhi ya watu, hii ni kutokana na watu wa benki mnapokwenda kumshawishi mteja kukopa mnatumia lugha laini, lakini hamtoi maelezo ya kutosha kuhusu riba ya mkopo," alisema Homera.

Alisema baadhi ya benki hazitoi elimu kwa wakopaji lakini wakati wa kudai maofisa wa benki wanatumia nguvu kubwa hali ambayo inawafanya wananchi kutopenda taasisi hizo.

Aliwataka wananchi kukopa kwa malengo na kuhakikisha mkopo unaelekezwa kwenye shughuli husika ili wanufaike badala ya kupata hasara na kushindwa kurejesha mikopo hiyo. Aliwakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwenda kuwekeza mkoani humo kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye hoteli ili kuhakikisha uchumi wa mkoa huo unakua.

Meneja wa Benki ya ACB tawi la Mbeya, Bahati Thomas, alisema walikutana na wateja wao ili kujenga uhusiano mzuri baina ya benki hiyo na wateja wake pamoja na kutambua kero za wateja ili kuongeza hamasa ya kuendelea kutumia benki hiyo.

Alisema katika kuboresha huduma za benki muda ni kipaumbele kwao hivyo wameongeza mtandao wa huduma za wateja ili kuwarahisishia wateja wao kupata huduma kwa wakati ikiwemo ulipaji wa bima mbalimbali kwa njia ya mkopo pamoja na riba zinaendana na wateja wao.

Kwa upande wake Meneja Mwandamizi wa Huduma Binafsi wa ACB, Emmanuel Mseti alisema benki hiyo inatekeleza wajibu wa kujitoa katika jamii kupitia sera yake ya kurudisha sehemu ya faida yake katika jamii.

Aliahidi kuwa benki hiyo itaendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo kuchangia ujenzi wa hospitali pamoja na kuhamasisha utunzaji wa mazingira.

"Benki yetu inashiriki vizuri katika shughuli mbalimbali za kutoa elimu ya fedha kwa vikundi na taasisi za wajasiriamali na pia tutakuwa sehemu ya wadhamini wa maonyesho ya Sikukuu ya Nanenane mwaka huu," alisema Mseti.

Aliahidi kuwa benki hiyo itachangia Sh. 5,000,000 ili kuungana na serikali katika dhamira yake ya kuboresha sekta ya kilimo nchini.



## Waziri ataka wanaotupa watoto kufichuliwa, kushtakiwa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, ameitaka jamii kutoa ushirikiano kwa kuwafichua wanaowatupa watoto ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Waziri Pembe aliyasema hayo jana katika Hospitali ya Mnazimmoja alipofika kumwangalia mtoto aliyeokotwa maeneo ya Kidongo Chekundu Mjini Unguja.

Alisema watu wenye ujauzito wanajulikana katika maeneo yao hivyo endapo itatokea mtu huyo haonekani tena na ujauzito wala kuwa na mtoto ni vyema kumripoti ili kufuatiliwa.

"Tusifichane jamani mitaani sote tunajuana, mtu akiwa na ujauzito utajua tu na akijifungua kama mtoto kafa pia tunapata habari, iweje hawa wanaowatupa watoto ndio tusiwajue? Jamani tushirikiane tuwafichue, kwani huu ni udhalilishaji," alisema Pembe.

Alisema kumtupa mtoto ni miongoni mwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa watoto na hivyo haviwezi kuvumiliwa.

Aidha, aliwataka wanawake wote kuacha tabia hiyo na mtu akijiona kutokuwa tayari kulea ni vyema kufuata wataalamu wa afya au kumpeleka mtoto sehemu husika, kwasababu kitendo cha kumtupa mtoto ni laana.

Naye Muuguzi Dhamana wa wodi ya watoto hospitalini hapo, Salama Ame Bakari alisema wamempokea mtoto huyo wa kiume mwenye uzito wa kilo 2.2 Juni 22, mwaka huu majira ya saa mbili asubuhi akiwa na majeraha kichwani na vidonda miguuni.

Alisema baada ya kumhudumia amekuwa katika hali ya kawaida na kwa sasa anaendelea vizuri, ambapo wataendelea kumpatia huduma hadi atakapokuwa katika hali nzuri na kukabidhiwa kwa wizara.

# Serikali kuboresha utendaji Tume ya Kurekebisha Sheria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema Serikali ya Zanzibar, imekusudia kuimarisha utendaji katika sekta mbalimbali ikiwamo Tume ya Kurekebisha Sheria.

Akiwasilisha ripoti ya Tume ya Kurekebisha Sheria katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana, Waziri huyo alisema, miongoni mwa hatua hizo ni kupitisha muundo wa utumishi wa tume hiyo kama hatua ya kuimarisha utekelezaji wa kazi.

Alisema tume imeanza utaratibu wa kuwasilisha ripoti mbele ya Baraza la Wawakilishi ili wafahamu maendeleo ya utafiti wa kisheria unaofanywa na tume hiyo.

Alisema maeneo 21 ya sheria yamefanyiwa mapitio na mapendekezo ya namna ya sheria hizo au maeneo hayo ya kufanyiwa marekebisho yamewasilishwa serikalini.

Suleiman alisema maeneo hayo yaliyofanyiwa kazi na tume yanajumuisha sheria zinazosimamia masuala ya uchumi kama vile mapitio ya Sheria ya Leseni ya Biashara, Namba 3 ya Mwaka 1983, Sheria ya Uvuvi, Namba 7 ya Mwaka 2010 na eneo la utatuzi wa migogoro ya ardhi. Alisema eneo linalopendekeza utungwaji wa sheria ya taasisi ya wahasibu, wakaguzi wa hesabu na washauri wa kodi na Sheria ya Utalii ya mwaka 2009 hasa katika eneo la Jeshi la Ulinzi wa Utalii.

"Eneo lingine lililozingatiwa na tume katika kufanya mapitio ni eneo la utawala bora. Katika eneo hili, tume imefanya mapitio ya Sheria ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Namba. 11 ya mwaka 2003, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Namba 4 ya mwaka 2015, Sheria ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi, Namba 1 ya mwaka 2012 na Sheria ya Kupambana na Utakatishaji wa Fedha Haramu, Namba 10 ya mwaka 2009," alisema.

Alisema pia tume katika mwaka wa fedha 2021/2022 iliangalia sheria zinazozingatia ushirikishwaji wa wananchi, kwamba miongoni mwa sheria zilizofanyiwa mapitio katika eneo hilo ni Sheria ya Jumuiya, Namba 6 ya Mwaka 1995 na Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, Namba 4 ya mwaka 2012.

Alizitaja sheria zingine ni Sheria ya Kinga, Uwezo na Fursa ya Baraza la Wawakilishi, Namba 4 ya mwaka 2007 na ya kufanya mapitio ya sheria zinazogusa maslahi ya wafanyakazi na wananchi kwa ujumla kama Sheria ya Utumishi wa Umma, Namba 2 ya mwaka 2011, Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Namba 15 ya mwaka 1986 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 3 ya mwaka 2015.

Alisema: "Pia Sheria ya Udhibiti wa Dawa ya Kulevya, Namba 9 ya Mwaka 2009, Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao, Namba 12 ya mwaka 2019, Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Namba 2 ya mwaka 2005 na Sheria ya Njia Mbadala za usuluhishi wa Migogoro, Sura ya 25".



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mysol, Godfrey Mugambi, akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa duka jipya la vifaa vya umeme wa jua na huduma za kampuni hiyo Zanzibar jana. Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na wananchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yashauriwa kuzipitia sheria za mwaka 1964

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi, Machano Othman Said, ameitaka serikali kuzifanyia marekebisho sheria zote ambazo zinatumika tangu kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiwalisha ripoti ya maoni ya kamati hiyo.

Alisema ni vyema Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar kuzipitia sheria za Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) na Sheria ya Mamlaka ya Maji Zanzibar ili kuona kama zinakidhi kutumika katika sekta ya nishati na madini.

Alisema kwa sasa sekta hizo zinatumia sheria hizo kwa maana kwamba hakuna sheria rasmi ambazo zilizoanzishwa kuendesha sekta hizo za nishati na madini.

Machano alisema ripoti yake imeeleza jukumu lake la kuziweka sheria katika lugha nyepesi ambazo zinaeleweka na kila mmoja katika jamii.

"Kwa mnasaba huo, tume inafanyakazi ya kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kuzifahamu sheria na kuzitekeleza ipasavyo, ili kuhakikisha elimu imemfikia kila mmoja, kamati inaipongeza tume kwa kuandaa vitabu ambavyo vitasaidia kufafanua matukio mahsusi katika jamii ikiwemo suala la ndoa na talaka, vizazi na vifo na usajili wa Mzanzibari mkaazi," alisema.

Aidha, alisema kamati inazitaka taasisi zote zenye kusimamia sheria na kutoa haki kwa jamii kuhakikisha zinatoa elimu ya kutosha kwa raia juu ya matumizi bora ya sheria.

Aidha, alisema kwa upande wa serikali inapaswa kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo yanayotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria kwa lengo la kuandaa sheria zilizobora ambazo zitatumia lugha zinazotambulika na wananchi pamoja na kuzifanya utekelezaji wake uwe rahisi na wenye kufahamika.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA DODOMA
SHAURI LA RUFAA ARDHI NA. 47/2023
TANZANIA POSTAL BANK PLC......MWOMBAJI
DHIDI
LAMECK ORGENES LYIMO......MJIBU MAOMBI
TULVIN INVESTMENT (T) LTD.........1ST NECESSARY PARTY
MIRAJI NYALANDU.........2ND NECESSARY PARTY
KWA: TULVIN INVESTMENT (T) LTD
POPOTE PALE ULIPO
YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA RUFAA NA. 47/2023
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu ya Tanzania, kanda ya Dodoma, mbele ya Mhe. Jaji F. R. Khalfan, wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya Jumanne tarehe 6/7/2023.

**HIVYO BASI;** Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO;** Hutafika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itavyoamua pasipo wewe au Wakili wako kuwepo.

**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15 Mwezi wa Juni, 2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA.

## NAFASI YA KAZI

KAMPUNI YA MADAWA ILIYOPO DAR ES SALAAM INATAFUTA SALES MAN. AWE ANAJUA KUENDESHA PIKIPIKI NA AWE NA LESENI.

PIGA SIMU NAMBA: +255 713 786 300

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

BY THIS DEED POLL I, the undersigned ALLY SAID SULE of P.O. Box.....Dar es salaam Tanzania DO HEREBY absolutely renounce and abandon the use of my former name of ALLY SAIDI and in lieu thereof assume the name of ALLY SAID SULE.

AND IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid, I hereby declare that I shall, at all times hereafter in all records, deed and instruments, in writings and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions whatsoever use and sign the said name of ALLY SAID SULE as my name in lieu of the former name of ALLY SAIDI renounced.

AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUEST all persons to designate and address me by such assumed name of ALLY SAID SULE only.

I, the said ALLY SAID SULE make this declaration conscientiously believing the same to be true and in accordance with the Provisions of Oaths, (Judicial Proceedings) and Statutory Declarations Act. 1966.

IN WITNESS WHEREOF I have executed this deed on the 6th June, 2023.



SIGNED AND DELIVERED by the said ALLY SAID SULE in my presence this 06th June 2023. DEPONENT

BEFORE ME:
Name: ELIAIKA RENATUS MMARI
Signature:
Address: 80184, DAR ES SALAAM
Date: 06TH JUNE 2023
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS.

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 67 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late**
**LAZARO KITUNDU LAZARO**

**By 1. DOROTHY LUDOVIC RUTAKYAMIRWA**
**2. ...................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **KASELE** day of **12 / 7 / 2023**
Dated at **Morogoro**, this **22** day of **06, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT

## KUPOTEA KWA CHETI



**RACHEL HENRICH BAISI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0225-0056 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia CAGLIERO GIRLS SEC. SCHOOL mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA : IRI/IRI/RB/203330/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DOMINIC PAULO SHAIBI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia BOZA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL mwaka 1987. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/CEN/RB/216583/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BASHIRU SHILLA JUMA,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari aina ya TOYOTA PRADO yenye no za Usajili T469AMC, CHASSIS NO KZJ780007149, MODEL NO KZJ78. Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI:
**DOD/DOD/RB/300032/2022**

***OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mobile: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, Website: www.ippmedia.com***

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# LUWASA yaelemewa na madeni ya umeme

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAMLAKA ya Maji na Usafi wa Mazingira mjini Lindi (LUWASA) inadaiwa jumla ya Sh. milioni 466 na Shirika la Umeme (TANESCO) na kuwa hatarini kukatiwa huduma hiyo huku uwezo wa kulipa deni hilo ukiwa mdogo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa (LUWASA), Jamila Keya, alisema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya mamlaka hiyo na changamoto zinazoikabili.

Viwango vilivyopendekezwa na mamlaka hiyo ni pamoja na kuunganishiwa upatikanaji wa huduma kwa wateja, mita za ujazo na kurejeshewa wateja huduma ya maji pale wanapositishiwa kwa kosa la kuchelewa kulipa bili.

Akiwasilisha mapendekezo hayo, Jamila alisema mamlaka inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwamo gharama kubwa za uzalishaji maji unaofanyika kupitia vituo 10 vilivyopo vya kusukuma maji unaofikia wastani wa Sh. milioni 50 kila mwezi.

Alisema deni hilo la Sh. milioni 466 linalodaiwa TANESCO ni la kipindi cha kuanzia mwaka 2017/2018 hadi Aprili mwaka huu.

Alizitaja changamoto zingine kuwa ni pamoja na uchakavu wa mita za wateja, uhaba wa vitendea kazi, ufinyu wa mtandao wa usambazaji maji, mabomba ya kusambazia maji na upungufu wa watumishi.

Alisema kutokana na changamoto hizo mamlaka hiyo ilipendekeza kuongeza ada kwa watumiaji wa majumbani kutoka Sh. 1,600 hadi Sh. 4,690, taasisi kutoka Sh. 1,700 hadi 4,993, biashara kutoka Sh. 2,100 hadi Sh. 6,150 na viwanda kutoka Sh. 2,200 hadi Sh. 6,449 kwa ujazo.

Wakichangia katika kikao hicho, watumiaji wa huduma hiyo, Baraza la Ushauri la Serikali (GCC), watumiaji huduma zinazodhibitiwa na EWURA CCC, wamepinga viwango hivyo na kuitaka LUWASA kufikiria upya na kupunguza viwango pendekezwa ili viwe kati ya Sh. 1,800 na Sh. 2,000 kwa ujazo.




Meneja wa Tawi la Benki ya Tanzania Commercial (TCB) Kigamboni, Lameck Buberwa, akimkabidhi Kaimu Mkuu wa Soko la Samaki Feri, Ally Kasembe, vifaa vya usafi ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi kwa Umma, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YPC yasisitiza majukwaa kupata hoja za wananchi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa Shirika la Vijana la Youth Partnership Countrywide (YPC) la Kibaha, Israel Ilunde, amesema majukwaa ni sehemu muhimu katika kuwezesha wananchi kufikisha kwa urahisi serikalini vikwazo wanavyoikabili na kushughulikiwa haraka.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki mjini hapa, Ilunde alisisitiza umuhimu wa majukwaa hayo baada ya kufanyika kwa Jukwaa la Ufahamu lililoandaliwa na taasisi hiyo, likijikita katika changamoto za mawasiliano ya simu za kiganjani.

Mkurugenzi huyo alisema majukwaa ya taasisi hiyo ambayo yatakuwa yanafanyika kila mwezi, ni sehemu muhimu ya wananchi kushiriki kupata elimu na kufikisha vikwazo vilivyopo katika maeneo yao ambavyo baadaye vinafikishwa kwa walengwa kwa ajili ya utatuzi.

"Leo katika jukwaa letu la mwezi, tulikuwa tukizungumzia changamoto za mawasiliano ya simu na walikuwapo Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano, kila lililoelezwa hapa litafikishwa sehemu husika kwa kutafutiwa ufumbuzi na kila mwezi kutakuwa na mada nyingine.

Kiongozi huyo alisema jukwaa hilo ni mwendelezo wa majukwaa yanayoandaliwa na taasisi hiyo ambayo yamekuwa yanafanyika miaka ya nyuma kwa kuwakutanisha wananchi, hasa vijana na kutoa elimu katika masuala mbalimbali ambayo imekuwa na mafanikio kwa kupata viongozi kutoka kwa washiriki.

Katika Jukwaa hilo mwandishi wa habari mkongwe, Ayoub Mtawazo, alisema baadhi ya watu wamekuwa wakivuruga mawasiliano kwa kuyatumia vibaya, jambo ambalo mamlaka husika inatakiwa ilifanyie kazi.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Ushauri la TCRA-CCC Mkoa wa Pwani, Jovina Mavoa, alisema elimu inayotolewa na jukwaa hilo itasaidia kupunguza malalamiko kwa watumiaji wa simu.

# Mradi DAWASA kutatua kero uhaba wa maji kituo cha afya

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Afya cha Chanika jijini Dar es Salaam kitaanza kupata majisafi na salama ya uhakika kuanzia mwishoni mwa mwezi huu baada ya kukamilika kwa mradi mkubwa wa maji.

Mradi huo umesimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ofisi ya Kisarawe.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Msimamizi wa Mradi huo, Erasto Mwakilulele, alisema hiyo ni kazi muhimu kwa kuwa inalenga kusaidia upatikanaji wa maji katika kituo hicho ambacho kwa muda mrefu wauguzi wamekuwa wakitumia maji ya chumvi.

Alisema mradi huo ni muhimu kwa lengo la kuboresha na kurahisisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wengi wanaohudumiwa katika kituo hicho cha Chanika.

"Tumeona umuhimu wa kutekeleza mradi huu wa kupeleka huduma katika hospitali kutokana na uhitaji mkubwa wa maji uliopo katika kituo hiki cha ya afya kinachotoa huduma kwa wakazi wengi wa Wilaya ya Ilala, mamlaka inatambua kuwa huduma ya majisafi ni muhimu sana katika utoaji wa huduma ya afya," alisema.

Alisema utekelezaji wa mradi umehusisha ulazaji wa mabomba makubwa ya inchi nne, tatu na mbili kwa umbali wa kilomita 1,550 kwenda kituoni huko.

"Mradi huu tunautekeleza kwa kutumia chanzo cha maji cha tangi la Kisarawe lenye ujazo wa lita milioni sita, ambalo litasambaza maji kwa msukumo mkubwa kwenda kituo cha afya," alisema.

Sambamba na hilo, alisema mradi utanufaisha pia wakazi wa mitaa mbalimbali inayopitiwa na mradi ambako jumla ya kaya 200 za mitaa ya Nyeburu, Nguvu Mpya na barabara ya Kilimahewa itanufaika.

"Mpaka sasa tumetekeleza mradi huu kwa asilimia 85, ambapo mwisho wa mwezi wa sita (Juni) huduma katika kituo cha afya kilichoko Chanika itaanza kupatikana," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Chanika, Pascal Nkii, alisema ukosefu wa huduma ya maji umekuwa ukisababisha matumizi makubwa ya fedha kwa watu binafsi.

Alisema ukosefu wa maji pia unaathiri uendeshaji wa mitambo ya afya, hivyo kulazimika kutumia gharama kubwa ya kununua maji ya mitaani ambayo wakati mwingine yanakuwa na chumvi.

Alisema kwa wastani kituo hicho hupokea wagonjwa 750 kwa siku, hivyo huwa wanapata changamoto hasa wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa bila majisafi na kuongeza kuwa mradi huo wa maji utakuwa mkombozi kwao.

Mwajuma Shomari, mkazi wa Chanika aliyepata huduma katika kituo hicho cha afya, alipongeza DAWASA kwa kuondoa changamoto ya ukosefu wa maji kituoni kwa kwa wamekuwa wanatumia maji ya chumvi kwa muda mrefu ambayo sio salama kiafya.

Alibainisha kuwa huduma ya majisafi katika hospitali ni muhimu sana, hasa kwa huduma ya mama na mtoto.

Alisema kuwa huduma ya majisafi itawasaidia sana wanawake na watoto wakati wa huduma za afya.

# BODI YA LIGI YATOA NENO KUMALIZIKA MSIMU 2022/23

Na Adam Fungamwango

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imetangaza rasmi kumalizika kwa msimu wa 2022/23 kwa mashindano yote nchini huku ikitoa pongezi kwa wadau mbalimbali kwa ushirikiano wa kufanikisha kuwa wa mafanikio.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi imewashukuru wadhamini, vyombo vya habari, mashabiki na wadau mbalimbali waliozifanya ligi walizokuwa wakizisimamia kumalizika salama, huku zikiwa za kuvutia.

**"Tunaishukuru serikali kwa kurahisisha masuala mengine ya kiuendeshaji na usimamizi wa ligi, serikali, imetengeneza mazingira bora salama kwa michezo ya ligi kuchezwa nchini huku klabu zetu zikisafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine bila vikwazo wala changamoto za kiusalama au miundombinu," ilisema taarifa hilo.**

Bodi imesema inaendelea na maandalizi ya msimu wa 2023/24 ambapo inahitaji ushirikiano wa wadau kwa kutoa maoni yao ili kutimiza lengo la kupata msimu bora zaidi.

Upande wa Ligi Kuu, Klabu ya Yanga imetwaa ubingwa wakati kwenye Ligi ya Championship, JKT Tanzania, KItayosce (Tabora United) na Mashujaa FC zikipanda Ligi Kuu, huku First League, TMA ya Arusha, Cosmopolitan ya Dar es Salaam na Stand United ya Shinyanga zikipanda hadi Ligi ya Championship.

MABAHARIA...




Wachezaji wa Timu ya Chuo cha Mabaharia, Mbaraka Uzia (kushoto) na Shedrack Kapau, wakiwania mpira wakati wa mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Geita Gold kusajili wapya 6

Na Saada Akida

UONGOZI wa Geita Gold FC, umesema utaongeza wachezaji sita wapya watakaowasajili kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha timu hiyo kwa msimu wa 2023/24 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Geita Gold inaenda kujaza nafasi ya kipa baada ya kuachana na Arakaza Macarthur, beki wa kati, kiungo mkabaji na washambuliaji wawili kwa ajili ya kuhakikisha inakuwa na kikosi imara.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Geita Gold FC, Saimon Shija, alisema wamefikia uamuzi huo baada ya kufanya tathmini ya msimu wa 2022/23 na kuifanyia kazi ripoti waliyoachiwa na aliyekuwa kocha wao, Felix Minziro.

Alisema mchakato wa usajili unaendelea kwa kuangalia wachezaji ambao watakuja kufikia malengo yao ya msimu ujao baada ya msimu uliopita kutoyafikia kwa nje ya nafasi tano za juu kwenye Ligi Kuu Bara.

"Msimu uliomalizika hatukufikia malengo yetu ya kumaliza kwenye nafasi tano za juu na tumeshuka hadi ya saba, baada ya kufanya tathmini na kuona tunatakiwa kufanya maboresho katika kila eneo ikiwa ni pamoja na kusajili katika nafasi hizo.

"Ili kufikia malengo yetu kwa msimu ujao lazima tufanye usajili mzuri pamoja na kuboresha benchi letu la ufundi kwa kuleta kocha ambaye analifahamu soka la Afrika vizuri," alisema Shija.

Aidha, kuhusu kutajwa aliyekuwa Kocha wa Kagera Sugar, Francis Baraza, anayetajwa kuchukuwa nafasi ya Minziro, Katibu huyo alisema wanahitaji kupata benchi la ufundi lililo bora na tayari wamepokea wasifu zaidi wa makocha 20 kutoka mataifa mbalimbali ikiwamo Ulaya, Afrika Mashariki na Kati pamoja na Tanzania.

"Kwa sasa hatuwezi kusema ni kocha yupi kwa sababu bado tunaendelea kupitia wasifu wa makocha hao, huyo mwalimu anayetajwa (Baraza) ni miongoni mwa waliotuma CV zao," alisema Shija.




# Tava yasifu viwango Ligi ya Taifa Wavu

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa Chama cha Mchezo wa Wavu Tanzania (Tava), umesema umeridhishwa na viwango vilivyoonyeshwa na timu shiriki kwenye Ligi ya Taifa ya mchezo huo ambayo inaendelea kwenye Uwanja wa Gwambina, Dar es Salaam.

Akizungumza na Gazeti la Nipashe jana, baada ya kumalizika michezo ya asubuhi Katibu wa Mashindano hayo, Riziki Godwin, alisema timu zote ambazo zimecheza zimeonyesha ushindani mkubwa.

"Timu zote ambazo tayari zimecheza, zimeonyesha ushindani mkubwa jambo ambalo tunaamini tutapata timu bora za taifa," alisema Godwin.

Aidha, aliwaomba wadau mbalimbali kujitokeza kuwaunga mkono kwa lengo la kufanya ligi hiyo iwe yenye ubora.

Katibu huyo alisema ligi hiyo itachezwa kwa mizunguko minne ambapo wa kwanza utamalizika Juni 30, wa pili utaanza Julai 17-28 huku mzunguko wa tatu na wa nne ukiendelea ifikapo Septemba mwaka huu.

Katika michezo ya ligi hiyo iliyochezwa jana, Jeshi Stars (Dar) iliichapa timu ya Korosho (Mtwara) seti 3-0 wakati timu ya Kampala (Dar) ikiichakaza NHIF ya Dodoma kwa seti 3-0 huku JKU (Zanzibar) ilikiifunga Pentagon (Arusha) seti 3-1.

Ligi hiyo inashirikisha timu 22 za Wanaume na Wanawake kutoka Tanzania Bara pamoja na Visiwani ambapo 12 ni wanaume 10 za wanawake.

Aidha, ligi hiyo imeelezwa ni maalumu kwa ajili ya kupata timu za taifa ambazo zitashiriki mashindano ya kimataifa yatakayoanza Agosti mwaka huu, ambapo wanaume watakwenda nchini Misri na wanawake wakielekea Cameroon.

Tayari Tava, imemtangaza Alfred Serengia kuwa Kocha Mkuu wa Timu za Taifa za Wavu kwa mkataba wa mwaka mmoja, ambaye kwa sasa anaifutilia ligi hiyo kwa makini ili kupata wacheza watakaounda timu za taifa.

**Ligi hiyo inashirikisha timu 22 za Wanaume na Wanawake kutoka Tanzania Bara pamoja na Visiwani ambapo 12 ni wanaume 10 za wanawake.**

## ZISIKUPITE

### GVARDIOL NA MAN CITY

KLABU ya Manchester City imewasilisha dau la euro milioni 90 kwa Josko Gvardiol, 21, wa RB Leipzig huku beki huyo wa Croatia akitajwa kama "mchezaji wa ndoto" ya Kocha Pep Guardiola. ***(Sky Sport)***

### JACKSON KUTUA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Villarreal na Senegal, Nicolas Jackson, 22, anatazamiwa kukamilisha uhamisho wa euro milioni 35 kwenda Chelsea baada ya kukamilisha uchunguzi wa afya katika klabu hiyo Jumapili. ***(Mail)***

### ARTETA ANA FURAHA

KOCHA Mikel Arteta, amesema anafuraha Arsenal na amepuuza ripoti zinazomhusisha na Paris St-Germain. ***(Marca)***

### GRAY ATAKIWA ARABUNI

KLABU ya Klabu ya Al-Hilal ya Saudi Arabia, inataka kumsajili winga wa Jamaica, Demarai Gray, 26, kutoka Everton, huku mazungumzo yakipangwa kufanyika wiki ijayo. ***(Mail)***

### MINA KUSAJILIWA FULHAM

MLINZI wa kati wa Colombia, Yerry Mina, 28, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Everton mwishoni mwa msimu huu, anatarajiwa kusajiliwa na Fulham. ***(Sun)***

### ZIYECH NAE ATAKIWA

KLABU ya Al-Nassr inatumaini kukamilisha dili la winga wa Chelsea kutoka Morocco, Hakim Ziyech, 30, mapema wiki hii, na kumfanya kuwa mchezaji wa nne kuondoka Stamford Bridge kwenda Saudi Arabia msimu huu wa majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

### WACHEZAJI 11 KUONDOKA UTD

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, ataruhusu wachezaji 11 kuondoka Old Trafford msimu huu wa majira ya joto huku akiomba kupata zaidi ya pauni milioni 100 kusaidia kubadilisha kikosi chake. ***(Sun)***

### KUDUS AWINDWA UNITED

MANCHESTER United inamtazama kiungo wa kati wa Ajax na Ghana, Mohammed Kudus, 22, baada ya kushindwa kufanya maendeleo na Chelsea kuhusu mpango wa kumnunua Mason Mount. ***(ESPN)***

### TUCHEL AMTAKA MOUNT

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, anatamani kuungana tena na kiungo wa kati wa England, Mason Mount, 24, ambaye alikuwa akimfundisha Stamford Bridge. ***(Guardian)***

### DE VEN ATAKIWA LIVER

KLABU ya Liverpool inajipanga kushindana na Tottenham Hotspur kumnunua mlinzi wa Uholanzi, Micky van de Ven, 22, ambaye yuko tayari kuondoka Wolfsburg msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### GULER ATAJA ZINAZOMVUTIA

KIUNGO wa kati wa Uturuki, Arda Guler, 18, anavutiwa na Arsenal, Liverpool, Real Madrid na Benfica. ***(Record)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KOULIBALY ATUA KUKIPIGA AL HILAL YA SAUDI ARABIA

**RIYADH,** Saudi Arabia

**Afunguka niko hapa na wale wanaofanya utukufu kwa sasa na siku zijazo...**

BEKI wa Senegal, Kalidou Koulibaly, amejiunga na Klabu ya Al Hilal ya Saudi Arabia kutoka Chelsea inayoshiriki Ligi Kuu England, klabu hizo mbili zilitangaza Jumapili.

**"Tutaendelea kuweka historia pamoja," ilisema taarifa ya Al Hilal kupitia kwenye ukurasa wake wa Twitter, pamoja na video fupi iliyomwonesha Koulibaly.**

Washindi hao mara nne wa Ligi ya Mabingwa Asia, walisema Koulibaly amesaini mkataba hadi mwaka 2026 bila kutoa maelezo yoyote ya kifedha.

Vyombo vya habari vya England viliripoti kwamba klabu hiyo ya Saudia ingelipa takriban pauni milioni 17 kwa ajili ya beki huyo wa kati.

"Niko hapa na wale wanaofanya utukufu kwa sasa na siku zijazo," alisema Koulibaly.

Koulibaly mwenye umri wa miaka 32, alifunga mabao mawili katika mechi 32 katika michuano yote akiwa na Chelsea baada ya kujiunga nao kutoka Napoli Julai mwaka jana.

Yeye ni mchezaji wa pili kuhamia Al Hilal kutoka Ligi Kuu England baada ya kiungo wa Ureno Ruben Neves kusajiliwa kutoka Wolverhampton Wanderers Ijumaa wiki hii.

Ligi ya Saudi, Pro League imekuwa ya kuvutia kwa wachezaji wa Ulaya tangu Cristiano Ronaldo alipohamia Al Nassr Januari.

Mabingwa wa ligi Al Ittihad walimsajili mshindi wa Ballon d'Or, Karim Benzema mapema mwezi huu, huku klabu hiyo pia ikithibitisha kuwa kiungo wa zamani wa Chelsea, N'Golo Kante, anajiunga nao.

Al Hilal ndio klabu iliyopambwa zaidi nchini Saudi Arabia na Asia, ikiwa imeshinda mataji 66, na wanashikilia rekodi ya mataji ya Ligi na Mabingwa wa Asia wakiwa na mataji 18 na manne mfululizo.

# UNITED KUTAFUTA MBADALA WA MOUNT




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inafikiria kulenga shabaha nyingine ya kiungo kwa sababu ya hofu kwamba mazungumzo na Chelsea kuhusu Mason Mount yanakwama, kwa mujibu wa ESPN.

United wamekataliwa ofa tatu za kumtaka Mount, huku ya hivi karibuni zaidi ni ile ya pauni milioni 55.

Chelsea wamedokeza kuwa watakubali ofa ya pauni milioni 58 pamoja na nyongeza nyingine ya pauni milioni 7 na kupendekeza mazungumzo ya ana kwa ana katika juhudi za kusuluhisha hali hiyo.

Hata hivyo, United wanaamini kwamba thamani ya Mount ni sawa kutokana na kwamba mchezaji huyo wa Kimataifa wa England amebakisha mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake na ameifahamisha Chelsea kuhusu nia yake ya kuhamia Old Trafford.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba ofa ya hivi punde ya United kwa Mount inabaki mezani, lakini maswali yamekuwa juu ya kupatikana kwa walengwa wengine, pamoja na kiungo wa Brighton Moises Caicedo, Mohammed Kudus wa Ajax na Taylor Booth wa FC Utrecht.

United wanafanya kazi ndani ya bajeti kali msimu huu wa majira ya joto pamoja na kiungo na kocha Erik ten Hag pia angependa kusajili mshambuliaji na kipa.

Kutokuwa na uhakika juu ya mustakabali wa David de Gea kunamaanisha fedha zinaweza kutumika kumsajili golikipa mwingine.

# Arteta ataja Arsenal ilipopotea

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema roho ya klabu hiyo "ilikuwa imepotea" kabla ya kuchukua uongozi mwaka 2019.

Arteta alikuwa kocha msaidizi wa Pep Guardiola katika Klabu ya Manchester City kwa miaka mitatu kabla ya kujiunga na Arsenal na kuwafanya washindani wa ubingwa wa Ligi Kuu msimu uliopita.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 41, alisema alihisi ukosefu wa uhusiano kati ya wachezaji wa Arsenal na mashabiki wakati City ilipocheza pale Emirates na alikuwa amedhamiria kubadilisha mambo.

"Hii ilianza zaidi miaka mitatu iliyopita. Nilikuwa msaidizi wa Pep kule City, tulicheza dhidi ya Arsenal na nikaona kwamba roho ya klabu ilikuwa imepotea," alisema Arteta akiliambia gazeti la Marca.

"Haikufurahishwa, haikuhisiwa. Nilijua kwamba kulikuwa na chaguo, muda mfupi baadaye, kuwa kwenye benchi nyingine na nilijua kuwa klabu hii ni kubwa sana kwamba ilipaswa kuunganisha timu na mashabiki.

"Imekuwa vigumu kufanya hivyo, na sasa ninajisikia furaha. Tuna utambulisho wazi, kuna muungano na tumejaa nguvu. Hilo ndilo jambo kubwa zaidi. Kuanzia juu hadi chini, wote wanasukuma upande mmoja."

Msimu uliopita, timu ya Arteta ilikaribia kushinda ligi kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2004, lakini ikamaliza katika nafasi ya pili nyuma ya City.


Arteta alisema kuwa majeraha pamoja na sare za gharama kubwa dhidi ya Liverpool, West Ham United na Southampton zilikuwa muhimu kwa mwisho mbaya wa Arsenal kwenye kampeni.

"Hadi leo, bado inaniuma sana kutoshinda Ligi Kuu baada ya kukaa kwa miezi 10 kupigana na City," aliongeza.

"Sare hizo tatu mfululizo zilituadhibu, na maafa yote yaliyotokea. Kulikuwa na majeruhi watatu au wanne kwa wachezaji muhimu na kutoka hapo, kila kitu kilikuwa kigumu.




# Silva awindwa Saudi Arabia




**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester City, Bernardo Silva, anasakwa na timu ya Al Hilal ya Saudi Arabia.

Mkataba wa Silva na Man City unatarajiwa kumalizika mwaka 2025 na klabu hiyo iko mbioni kumwongezea mkataba mwingine, huku akiwa na ofa kibao mezani.

Mabingwa wa Ufaransa Paris St-Germain (PSG) nao pia wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, wakati Barcelona imekuwa ikihusishwa na Mreno huyo kwa miaka miwili iliyopita.

Hata hivyo, klabu zote zinaweza kufunikwa na mshahara mnono utakaoupata Silva endapo atakubali kutuwa Al Hilal ya Saudi Arabia.

Al Hilal yenye maskani yake Riyadh, ambayo pia imemsajili Ruben Neves kutoka Wolves, imekuwa ikifanya kila jitihada kutaka kumsajili Silva.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno amehusika katika mafanikio ya Man City kutwaa taji la Ligi Kuu chini ya Kocha Pep Guardiola baada ya kujiunga na klabu hiyo mwaka 2017.

Aliisaidia klabu hiyo kutwaa mataji matatu msimu huu, likiwamo lile la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu na FA.

Tayari wachezaji wenye majina makubwa wameshatua katika klabu za Saudi Arabia.

Mshambuliaji wa Kimataifa wa Ureno, Cristiano Ronaldo alijiunga na Al Nassr Januari.

Kiungo Mfaransa, N'Golo Kante naye pia amekubali kujiunga na mabingwa wa ligi ya nchi hiyo, Al-Ittihad baada ya kumalizika kwa mkataba wake Chelsea, huku Mfaransa mwenzake, Karim Benzema naye pia alisaini katika klabu hiyo.

## Simba, beki Mcameroon kimeeleweka

INATOKA UKURASA 24

wapya.

"Tukimalizana nao, tutakuja na watu wa benchi la ufundi na baada ya hapo tutaanza sasa kushusha vyuma kimoja baada ya kingine," alisema.

Ikumbukwe kuwa klabu hiyo kwa sasa haina kocha wa viungo, mtaalamu wa misuli na kocha wa magolikipa baada ya kuachana nao hivi karibuni.

Walioondoka ni Chlouha Zakaria aliyekuwa kocha wa magolikipa, Kelvin Mandla, kocha wa viungo na mtaalamu wa viungo, Fareed Cassim.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema wachezaji Joash Onyago na Ismael Sawadogo ni kati ya wachezaji ambao Simba inataka kuachana nao, lakini bado wana mkataba, hivyo mazungumzo bado yanaendelea.

## Gamondi apewa rungu Yanga SC

INATOKA UKURASA 24

"Tumefanya usajili mzuri, wachezaji tunaowaleta wanajua mpira, tumeshusha watu wa ukweli kulingana na mahitaji yetu ya msimu ujao kuendelea tulipoishia msimu huu iwe kutetea mataji yetu yote na kuleta Kombe la Afrika katika ardhi ya Tanzania," alisema Kamwe.

Aliongeza kuwa wamefanya usajili mkubwa na kusisitiza kuwa mchezaji atakayekuja kuvaa jezi namba sita ni balaa kwa kuwa anajua mpira na amefanya vizuri katika klabu aliyotoka.



# COASTAL YAVUNJA BENCHI LA UFUNDI, YATANGAZA KAMATI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union imepitisha bajeti yake ya kuelekea msimu ujao wa mashindano, ikiunda kamati mbili za mipango na usajili, huku ikivunja benchi lake la ufundi.

**Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Omari Ayoub, amesema hayo yote yamefanyika kwenye Mkutano Mkuu uliofanyika juzi jijini Tanga.**

Amesema pamoja na mambo mengine, lengo la mkutano huo lilikuwa ni kupitisha bajeti ya msimu ujao wa mashindano kwa klabu hiyo.

"Tulikuwa na mkutano mkuu kupitisha bajeti yetu ya msimu ujao ambayo itakuwa dira ya klabu yetu, lakini kwenye mkutano huo tumevunja benchi la ufundi la 2022/23, hivi karibuni tutatangaza kina nani tutakuwa nao, pia tumeunda kamati mbili, moja ya mipango itakayoongozwa na Salim Bawazir, pia kuna kamati ya usajili ambayo itaongozwa na Hamisi Salehe na wenzake," alisema katibu huyo.




Alisema baada ya mkutano huo, kitakachofuata sasa ni kuendelea kuacha baadhi ya wachezaji na kisha kufanya usajili bora kuelekea msimu ujao.

"Kuhusu kocha mkuu, tunatazama ndani ya nchi na nje, mazungumzo yanafanyika, lolote linaweza kutokea, na kwenye usajili tuna uhakika tuliowapa dhamana watatusajilia wachezaji wenye viwango vya kuichezea klabu yetu kubwa kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati," alisema Omari.

Hata hivyo, tetesi zinadai kuwa klabu hiyo huenda ikamchukua kocha wa zamani wa Simba, Goran Kopunovic raia wa Serbia, au Javi Martinez raia wa Mexico.

Coastal ambayo imeponea chupuchupu kushuka daraja na kwenda kucheza mechi za mchujo 'play off', ilikuwa chini ya kocha Fikirini Elias na Msaidizi wake, Joseph Lazaro.

Tayari klabu hiyo imeachana na wachezaji Joseph Zziwa raia wa Uganda, anayecheza nafasi ya ulinzi, Mrundi Emery Nimuboma, aliyewahi kuichezea Simba miaka ya nyuma, pamoja na golikipa raia wa Comoro, Mahmoud Mroivili.



Wachezaji wa timu ya vijana ya Mtibwa Sugar U-20, wakishangilia moja ya mabao yao, dhidi ya Mbeya City katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara chini ya umri huo msimu huu, ikiwa mechi yao ya kwanza iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na kushinda mabao 5-0.

# *Simba, Yanga hoi Ligi U-20, Mtibwa, Geita zatinga robo*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za vijana chini ya miaka 20 za Simba na Yanga, zinakutana na wakati mgumu kwenye Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) chini ya miaka hiyo, huku Mabingwa Watetezi, Mtibwa Sugar na Geita Gold zikisonga mbele kwenye hatua ya robo fainali.

Wakati Yanga ikiburuza mkia kwenye Kundi B, Simba inakamata nafasi ya tatu Kundi D, hivyo zikiwa na nafasi finyu ya kusonga mbele.

Yanga haina pointi yoyote ikiwa imecheza mechi mbili na kupoteza zote, Simba ikicheza mechi mbili, ikipoteza moja na sare moja. Mtibwa Sugar ambayo ni mabingwa watetezi, imecheza mechi zote tatu na kushinda, ikitinga hatua ya robo fainali na pointi zake tisa, ikifunga mabao 10 na kuruhusu moja tu kwenye Kundi A.

Geita Gold nayo imesonga mbele Kundi C kwa kutinga hatua ya robo fainali ikishinda mechi zote tatu, ikifunga mabao sita na kufungwa moja tu, ikikusanya jumla ya pointi tisa.

Timu hizo mbili ndizo pekee zimepita, lakini Kundi B na D bado inategemea matokeo ya mechi zitakazochezwa.

Kundi B linaongozwa na Prisons yenye pointi sita, ikifuatiwa na Dodoma Jiji yenye pointi nne.

Kivumbi kiko kwenye Kundi D ambapo Azam FC inaongoza kwa pointi sita ikicheza mechi mbili, Ihefu ikiwa kwenye nafasi ya pili ikiwa na pointi tatu, huku Simba iliyo kwenye nafasi ya tatu na Kagera Sugar zote zina pointi moja.


Kwenye kundi hili msimamo wake ulivyo ni kwamba timu yoyote kati ya nne inaweza kwenda robo fainali.

Kwa mujibu wa TFF, robo fainali inatarajiwa kupigwa kuanzia kesho kwa timu zitakazoshika nafasi mbili za juu kwenye kila kundi, nusu fainali ikipigwa Ijumaa na fainali kuchezwa Julai 2, mwaka huu.

# Michezo

Jumanne Juni 27, 2023

Nipashe

Silva awindwa Saudi Arabia UKURASA 22

# Simba, beki Mcameroon kimeeleweka

## ●●● Milioni 359 zakubalika kumng'oa fundi wa kukaba Coton Sport, yenyewe yasema...

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Simba imesema imemaliza awali ya kwanza ya wachezaji iliyowaacha kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano, na sasa inakuja na ya pili ambayo itakuwa ni kwa wachezaji watakaowatoa kwa mkopo kwenda klabu zingine.

**Hata hivyo, wakati ikieleza hayo, habari kutoka Ghana zimedai kuwa Klabu ya Cameroon, imekubali kumuuza beki wake wa kati Che Fondoh Malone (24), kwa Klabu ya Simba baada ya kukubaliana na dau lililopelekwa mara ya pili.**

Kwa mujibu wa magazeti, na vyombo vya habari vya online nchini Ghana, Klabu ya Coton Sport FC imekubaliana na Simba juu ya kumuuza beki wao kisiki wa kati, Malone Junior.



Awali, klabu hiyo ilikataa ofa ya kwanza, lakini Simba ikapeleka ya pili ambayo imekubaliwa, hivyo kumnunua kwa kuvunja mkataba, ikilipa kiasi cha dola za Kimarekani 150,000, ambazo ni sawa na Sh. milioni 359.5 za Tanzania.

Tayari Simba ilishakubaliana na mchezaji kuhusu mkataba, mshahara na mambo mengine binafsi ya kimkataba.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema kimya ambacho wanachama na mashabiki wa Simba wamekiona wiki hii bila ya kuona 'thank you' yoyote ni kwa sababu wapo kwenye mazungumzo na baadhi ya wachezaji watakaotolewa kwa mkopo pamoja na wale ambao wanataka kuvunja nao mikataba.

"Hatujamaliza, ila kimya ambacho kimeonekana wiki hii ni kwa sababu tumemaliza wachezaji ambao tumewaacha, hatutokuwa nao msimu ujao na wamemaliza mikataba yao, lakini awamu ya pili itafuata kwa wachezaji ambao tutawatoa kwa mkopo kwenda klabu zingine, kwa sasa tupo nao katika mazungumzo, huwezi kutoa tu hivi hivi bila kumshirikisha. Tukishakubaliana nao, basi mtaona tu tena taarifa zetu za mfululizo kuwa fulani tumempeleka kwa mkopo," alisema Ahmed.

Mbali na hilo, alisema wapo wachezaji ambao klabu inataka kuachana nao, lakini bado wana mkataba, nao pia wako kwenye mazungumzo nao ili waachane kwa usalama na amani.

"Kuna wachezaji ambao wana mikataba, lakini klabu haitaki kuendelea nao, tuko nao kwenye mazungumzo ya mambo mbalimbali, ikiwamo kuwalipa fidia na yakimalizika nao pia tutawaweka hadharani kama wale wa kwanza," alisema.

Ahmed ambaye amerejea ofisini baada ya kupumzika kwa siku kadhaa kutokana na msiba wa baba yake mzazi, alisema wakishamaliza wachezaji wote, kitakachofuata ni kutambulisha watu wapya wa benchi la ufundi, kabla ya kutangaza wachezaji

INAENDELEA UKURASA 23



Che Malone

## Gamondi apewa rungu Yanga

**Na Saada Akida**

BAADA ya Yanga kumtangaza, Miguel Angel Gamondi kuwa kocha wao mkuu kuelekea msimu mpya, uongozi wa klabu hiyo umesema umempa jukumu zima la usajili kwa kushirikiana na mkurugenzi wa ufundi wa timu hiyo, kupitia tathmini ya ripoti ya kocha aliyepita kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha msimu wa 2023/24.

Yanga wamemtambulisha Gamondi kuchukuwa nafasi ya Nasreddine Nabi, ambaye ameachana rasmi na kikosi hicho baada ya kupata ofa ya kuinoa Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema wako makini katika usajili wa wachezaji wapya kwa kumshirikisha kocha mpya kwa kufuata matakwa ya timu yao kuelekea msimu ujao wa mashindano.

"Bahati tuliyopata ni kocha mwenye uzoefu mkubwa wa soka la Afrika, viongozi wamezingatia falsafa ya Gamondi kwa kuboresha kikosi chetu, hakuna mchezaji wa Yanga aliyesajiliwa kwa 'Chupli Chupli'," alisema Kamwe.

Alisema usajili unafanywa kwa kuangalia ripoti ya mwalimu aliyepita Nabi ambayo imekabidhiwa kwa mkurugenzi wao wa ufundi na sasa watashirikiana vizuri na kocha Gamondi ili kuona ni aina gani ya wachezaji watakaosajiliwa.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >